# *Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua*

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi kwa ajili ya maombi. Wakati wimbo huu unapokuja kwa utamu kupitia maikrofoni hizi, *Amini Tu*, sijui kama tuna haja, usiku wa leo, ambazo tungetaka zijulikane kwa Mungu. Huku mikono yetu imeinuliwa, tunaahidi tutaamini tunapoinua mikono yetu. Bwana abariki.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunakukaribia Wewe, katika Jina la Bwana Yesu, kwa sababu kwamba Wewe umeahidi, kama tukiifanya namna hii, kwamba Wewe ungetusikia. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utapokea kile tunachohitaji, katika ufahamu Wako, Bwana, na utatupa thawabu kulingana na imani yetu. Tunajua utatupa, kwa kuwa uliahidi. Zipo haja nyingi. Mikono mingi iliinuliwa; wangu, pia, Bwana. Ninaomba ya kwamba Wewe utakutana tu nasi, usiku wa leo, na kutuonyesha jinsi itupasavyo kuishi na kile kitupasacho kufanya kuwa na imani Kwako. Jitwalie utukufu kutoka kwa ibada hii, Bwana, tunapojikabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

3 Don, u hali gani? Hakika nimeshangaa, usiku wa leo, kuona wengi wa marafiki zangu wameketi hapa jukwaani pamoja nami. Ndugu Lee Vayle alikuwa mmoja wa mameneja. Ndugu . . . Vema, siwezi kulitamka hilo jina la Kijerumani, Hierholzer. Ninalichanganya kila wakati. Ndugu Don Ruddell na ndugu wote hapa, kila mtu, ninafahamiana nao wote, kwa hiyo nina furaha sana kuwa nao hapa usiku wa leo ku—kuomba pamoja nasi wakati tukihubiri Neno, tukiombea wagonjwa.

4 Sasa, nafikiri, kesho usiku, na halafu Jumapili alasiri, kurudi huko, kisha Jumamosi usiku inapaswa kuwa mahali pengine. Je! mmekuwa mkiomba leo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sawa.

5 Ninasikitika niliwacheleweshaa, jana jioni. Lakini palikuwa ni mahali pageni, kila kitu kigeni, na mnajua huchukua muda kidogo ili kuzoeana. Kama nilivyozoea kusema, samahani tamshi hilo, "Kuondolea mbali mizuka yote, tunapopata kufahamiana, kusudi sisi . . . hisia zote za kiajabu."

6 Wakati mwingine mnakutana mahali. Loo, si kuudharau ukumbi huu, bali, unaona, si mikutano ya kidini kila mara, nadhani, inayofanyika hapa. Ni kila namna ya matumizi. Na humo ndani, haijalishi linavyoonekana la kiajabu, bali kuna

roho ya kila kitu. Kama huna roho ndani yako, umekufa. Na watu wenye roho mbalimbali hukutanika pamoja.

7 Yesu asingeliweza kuponya miongoni mwa kundi kama hilo. Alikuja katika nchi Yake mwenyewe, nao hawakumwamini, Naye asingeweza kufanya kazi kuu huko. Siku moja ilimbidi kuongoza m—mtu aliyekuwa kipofu, kote kutoka nje ya mji, kabla hajaweza kumfanya a—aone, na kupata wake. Na mmoja na kusikia kwake.

8 Mnaona, wakati mwingine inawabidi kuja pamoja ambapo waaminio wanajumuika pamoja na kuamini. Na mahali hapa pamewekwa wakfu sasa kwa ibada ya Bwana Yesu Kristo. Basi ni kanisa sasa, ni kanisa tu kadiri ambavyo. . .Popote ambapo watu wa—wanakutanika pamoja, hilo ndilo kanisa. Kwa hiyo sasa, usiku wa leo, sisi kwa kweli, tunajisikia, ni watu waliojaliwa sana sana, kuwa hapa usiku wa leo, kukutanika pamoja nanyi nyote, ku—kuomba na kumtambua Yesu Kristo miongoni mwetu.

9 Sasa, mwajua, Wapresbiteri wana ninii nyingi za. . . ama Waepiskopolia, ninaamini ndivyo, juu chini, juu chini; kusimama na kusema jambo, unaketi chini; simama na kusema jambo, unaketi chini. Nami nitawaomba msimame tena ninapolisoma Neno.

10 Katika Luka, mlango wa 24, kama mtasikiliza kwa makini sasa. Ni Maandiko marefu kweli. Ningependa kuanza na kifungu cha 13 cha Luka 24.

> *Na, tazama, siku ile ile wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili.*
>
> *Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yote yaliyotukia.*
>
> *Ikawa katika kuzungumza na. . .kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao.*
>
> *Macho yao yakafumbwa wasimtambue.*
>
> *Akawaambia, Ni* maneno *gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea, huku mmekunja nyuso zenu?*
>
> *Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je! wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo. . .siku hizi?*
>
> *Akawauliza, Mambo gani? Wakamwambia, mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote;*

*Tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulibisha.*

Nasi tulikuwa tukitumaini *ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo;*

*Tena,. . .wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha, waliokwenda kaburini asubuhi na mapema,*

*Wasiuone mwili wake; wakaja wakasema ya kwamba wametokewa na malaika waliosema kwamba . . .yu hai.*

*Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo . . .kama wale wanawake walivyosema, ila yeye hawakumwona.*

*Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote yaliyoyasema* maandiko*!*

*Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na* kuingia *katika utukufu wake?*

*Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza. . .katika ma—maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.*

*Wakakikaribia kile kijiji* walichokuwa *wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele.*

*Wakamshawishi wakisema, Kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa nao.*

*Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki,. . .akawapa.*

*Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao.*

*Wakaambiana, Je!* Mioyo *yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia* maandiko?

11 Hebu na tuombe. Bwana Yesu, tunajua kwamba hii ni kweli. Hakuna kitu chochote ulimwenguni kilicho kweli zaidi ya Neno Lako. Hakuna chochote ulimwenguni kilicho kikuu zaidi ya Neno Lako. Nasi tunaomba kwamba Wewe utatufunulia hadithi hii, mioyoni mwetu usiku wa leo, na utaifanya sehemu hii ya Maandiko kujirudia tena, usiku wa leo, kusudi tuweze kumtambua Bwana Yesu kama walivyomtambua. Ila tu, walimtambua siku mo—moja baada ya kufufuka kwake, na sasa jalia tumtambue baada ya miaka elfu mbili. Tunaomba katika Jina la Yesu na kwa utukufu Wake. Amina.

Ketini.

12 Asanteni kwa ishara ndogo ya makaribisho nyuma ya ukumbi wa kanisa.

13 Somo langu usiku wa leo lilikuwa: *Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua.*

14 Sasa mandhari yetu, usiku wa leo, ni Pasaka ya kwanza. Siku ile yenye giza kuu ya kusulubishwa ilikuwa imepita. Bwana wetu Yesu alikuwa amekuja ulimwenguni na alikuwa amejitambulisha Mwenyewe kikamilifu kuwa ni Mwana wa Mungu. Maandiko yote, yaliyokuwa yakimhusu, Yeye alikuwa ameyatimiza. Hata saa za mwisho msalabani zilikuwa zimetimizwa. Sasa ufufuo ulikuwa umekuja, ambao uliahidiwa pia. Lakini watu katika siku hiyo walikuwa kwa namna fulani kama tulivyo sisi, leo hii. Walikuwa na, katika shauku za kile ambacho walikuwa wakiona, cha kimbinguni, na kadhalika, walikosa kutambua Maandiko yote yaliyomhusu. Walikuwa wametambua baadhi Yake, na kuamini, na baadhi Yake hawakutambua.

15 Nafikiri hiyo inafanana kabisa na leo hii, kwamba mara nyingi tutapokea baadhi ya mambo ambayo Yesu amesema, bali si mambo yote aliyosema. Watu wakati mwingine wanafikia, kusema, "Vema, tunaamini *Hili*, bali hatuamini *Hili*." Vema, huwezi kuamini *Hili* pasipo kuamini *Hili*. Unaona, lazima uliamini lote. Ama yote ni Mungu, au si Mungu hata kidogo. Basi kwa hiyo halina budi kuwekwa sawasawa, mahali pake.

16 Na kama nilivyosema jana jioni, Mungu amegawa hilo, Andiko Lake, tangu mwanzo, kabla hapajakuwako na wakati, wakati Yeye alipokuwa wa Milele. Yeye wote. . . Yeye ni Yule wa Milele, na ndipo mambo haya yanayotendeka sasa ni sifa tu za mawazo ya Mungu. Kwanza kabisa, halina budi kuwa ni wazo, na kisha Neno. Nalo Neno, wazo likitamkwa, ni Neno. Halafu basi, Hilo likinenwa, halina budi kutukia. Na kitu hicho chote ni Mungu akijifunua Mwenyewe katika sifa Zake, halafu Mungu akifanyika mwili, awezaye kuguswa, tunayeweza kumzungumzia, kusema naye, katika Mwili Wake wote wa Kanisa na kila kitu.

17 Kwa hivyo, jina lako lilikuwa katika mawazo Yake. Hivyo ndivyo ulivyo na Uzima wa Milele. Huwezi kuwa Nao kwa njia yoyote nyingine. Kama una Uzima wa Milele, daima ulikuwako. Unaona? Wewe, la sivyo, huwezi tu kusema, "Vema, mimi ni mshiriki wa kanisa, ninafanya *hili*." La, bwana. Uzima wa Milele kamwe haukuwa na mwa-. . . Chochote kilicho cha Milele kamwe hakikuanza wala hakiwezi kwisha. Kwa hiyo wewe ulikuwa tu katika mawazo Yake, jina lako, kuwa wewe ni nani na kile ulicho. Hiyo ndiyo njia pekee ungeweza kuwa na Uzima wa Milele, maana ulikuwako daima.

18 Na wale, haijalishi kile walicho, wamekufa Milele, walikuwa wamekufa tangu mwanzo. Biblia ilisema, "Mwanamke anayeishi katika anasa amekufa huku yu hai." Kweli. Unaona, amekuwa mfu siku zote. Amekufa katika dhambi na makosa.

19 Na sasa kama ulikuwa katika kuhuishwa, kwenye mwanzo Wake, hicho ndicho Yeye alikuja kukomboa. Nalo jina lako liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, katika mawazo Yake, hapo mwanzo. Naye alikuja kukomboa majina yote yaliyoko kwenye Kitabu hicho; hakuna la ziada, hakuna hata moja la ziada; ni yale tu yaliyoko Humo ndani. Jina la mwisho likikombolewa, Yeye anakitwaa Kitabu Chake na kudai yale ambayo amekomboa.

20 Sasa, na lingekuwa ni ja—jambo la ajabu jinsi gani kama tusingeweza kuamini yote yaliyoandikwa katika Maandiko, kwani kitu hicho chote ni Neno la Mungu. Lote limevuviwa, kila sehemu Yake, nasi tunaamini kila sehemu Yake.

21 Sasa tamasha hii nzuri tuliyo nayo mbele zetu, usiku wa leo, ni Yesu aliyefufuka kutoka kwa wafu, katika majira ya kuchipua, akitembea huku. Kutoka kwenye kuchipua, ufufuo, Ua la kwanza kufufuka kutoka kwa wafu, Bwana wetu Yesu! Alikuwa ndiye Malimbuko ya wale waliolala. Ua la Pasaka lililochipuka, Lile la kwanza lililoinua kichwa chake baada ya usiku wa manane baridi wenye giza na dhambi; Yeye alikuwa amelipa gharama ya dhambi, ndipo Mungu akamfufua kwenye siku ya tatu. Tunaamini hilo kwa moyo wetu wote, kwamba Mungu alimfufua siku ya tatu, kulingana na ahadi Yake. Nasi tunaamini hilo kulingana na Maandiko, kwamba Yeye alimfufua, siku ya tatu. Alikuwa Ndiye wa kwanza aliyefufuka kutoka kwa wafu, Malimbuko ya wale waliolala.

22 Na kuliwazia, ile dhiki kuu kupitia miaka elfu nne ambayo ulimwengu ulikuwa umepapasapapasa katika dhambi, wala hawakujua njia ya kutokea, Huyu hapa amerudi kutoka kwa wafu! Ni wakati wa jinsi gani, majira ya kuchipua! Kanisa linapaswa liwe limekuwa likiimba haleluya zenye utukufu. Lakini badala ya hiyo, walikuwa wakizunguka huku wakiwa na mioyo mizito, huzuni na kila kitu, kwa sababu walikosa kuamini yote aliyosema.

23 Na ni jambo lilo hilo usiku wa leo, kwa sababu wanakosa kuamini yote ambayo Yeye alisema na kuahidi. Hilo ndilo, kanisa liko katika hali kama hiyo usiku wa leo, lililomo, ni kwa sababu tumekosa kuamini yote ambayo Yeye alisema angefanya. Maandiko yote yanayomhusu Yeye, tunakosa kuyaamini yote. Tunalipiga kote, kulichanganyisha, na kuweka kitu kingine ndani Yake.

24 Kama tunaamini Kitu hicho chote, kungekuwako na chemchemi ya furaha katika nafsi zetu, kwa sababu tumefufuka na Yeye katika mfano wa kufufuka Kwake, sasa tumeketi katika mahali pa Kimbinguni katika Kristo Yesu, huku falme zote na mamlaka na giza zikiwa chini ya miguu yetu. Tuna haki, pamoja na Damu ya Yesu Kristo, Ishara yetu, kwamba tumenunuliwa na Mungu. Kwamba, Mungu amelipia ukombozi wetu, kupitia Yesu

Kristo, nasi tuna haki ya kuishikilia Ishara hiyo juu ya chochote tuombacho, na kukipokea. Mungu alisema hivyo! Hilo latosha. Laiti tungaliweza tu kuamini Maandiko yote!

25 Bali jambo lilikuwa ni kwamba, sehemu yenye huzuni, watu wengi waliomjua Yeye na kumpenda, hawakutambua kwamba Yeye alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu.

26 Ndivyo ilivyo leo hii! Watu wengi, ambao wanaamini na hata kufundisha kwamba Yeye alifufuka kutoka kwa wafu, wangali hawatambui Hilo. Kwa kweli hawawezi kufahamu. Na ni jambo li—lisiloaminika. Ni jambo lisilo la kawaida kabisa. Mambo yasiyo ya kawaida ndipo alipo Mungu, ikiwa ni kulingana na ahadi Yake.

27 Wengi walimpenda, na hawakujua. Lilikuwa kabisa ni jambo lisilo la kawaida kwao kuamini kile wale mashahidi waliotoka kaburini na kusema, "Tuliona kundi la Malaika, waliosema, 'Amefufuka kutoka kwa wafu.'" "Loo, vema, sisi . . . " Mnaona, kama wangaliangalia tu kwenye Maandiko; Yeye aliahidi hilo, kwamba angelifanya.

28 Na kama tu vile kwa Mafarisayo na viongozi wa kidini wa siku Zake, kama wangalikuwa tu wameangalia katika Maandiko, kama alivyosema kufanya. "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi," yanayowaambia kwamba Yeye ni Nani.

29 Basi ikiwa wanafunzi hao kwenye siku hiyo wangaliangalia tu kwenye Maandiko, wangalipata katika Maandiko kwamba Yeye aliahidi kufufuka tena. Naye Mungu aliahidi kumfufua, na Yeye alifanya hivyo. Hata hivyo, Neno Lake lililoahidiwa liliandikwa kwamba Yeye angewafanyia hilo. Neno lilisema kwamba angefufuka.

30 Alikuwa ameahidi hilo, bali hata hivyo walikuwa na huzuni na kuvunjika moyo, na kila kitu. Walidhani walikuwa wamepoteza kila kitu walichokuwa nacho, na kila kitu kilikuwa kimeshindwa. Nayo ilikuwa ndiyo saa yenye giza zaidi ambayo, nadhani, waliwahi kuona. Walikuwa na matumaini katika Yeye, na kumwamini Yeye, na kuona madhihirisho Yake makuu ya miujiza na ishara na maajabu, na mathibitisho yote ya Masihi. Ndipo basi kumwona akisimama pale na kufa, na kuwa na mate usoni Mwake, na, wakati, Yeye angeweza kutambua mawazo yaliyoko mioyoni mwa watu.

31 Lakini kama nikitaja hili kwa m—msemo wa kilimwengu, samahani. Lakini, "wakati ma—mambo yamesambaratika," hapo ndipo bado unaamini.

32 Walipomfunga kitambaa usoni, wale askari walevi, na kuweka kitambaa usoni Mwake, na kuchukua fimbo na kumpiga kichwani, kasema, "Sasa, tunasikia kwamba Wewe ni nabii. Kama Wewe ni nabii," nao wakapokezana fimbo hiyo mmoja

kwa mwingine, na kusema, "tuambie ni nani aliyekupiga. Tutaamini."

33 Mnaona, ilionekana kana kwamba a—a—alikuwa amenaswa katika mtego. Nao wakawazia, "Vema, kama wangesema lolote Kwa—Kwake, angewapofusha tu. Angewapiga wafe, kama wangesema chochote." Mnaona, hilo daima si kusudi la Mungu katika kutenda mambo. Mnaona?

34 Wakati Yeye alipokuwa msalabani, naye Kayafa na ku—kuhani wote walisema, "Kama Wewe ndiye Kristo, tuambie waziwazi. Shuka utoke msalabani, tutakuamini." Unaona, wasingeweza kuelewa kabisa jinsi ambavyo Mungu angeweza kamwe kuenda msalabani na kufa. Bali, hiyo ndiyo sababu Mungu alifanyika mwili, kusudi aweze kufa.

35 Mafarisayo walimpa sifa kuu zaidi aliyowahi kupewa, waliposema kwamba wengine Yeye asingeweza . . . "Aliwaokoa wengine, Mwenyewe hawezi kujiokoa." Hakika, hiyo ilikuwa ni sifa. Kama angejiokoa Mwenyewe, asingeweza kuwaokoa wengine. Ilimbidi kujitoa Mwenyewe.

36 Hiyo ndiyo sababu Mungu alifanyika mwili, kusudi afe, ili aweze kuteseka na kuchukua adhabu juu Yake Mwenyewe. Asingelifanya mradi tu alikuwa ni Yehova, katika roho. Mungu Baba, katika roho, asingeweza kulifanya. Bali wakati Mungu alipofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, Mwanadamu, basi aliweza kuonja mauti, na anachukua adhabu ambayo alikuwa ameweka juu ya wanadamu wote. Aliichukua Mwenyewe, na kulipa gharama.

37 Hata hivyo, Neno Lake lililoahidiwa lilikuwa limeahidi ufufuo huu, bali hawakuelewa kwamba ungekuwa hivyo. Wasingeweza kabisa kuufikia. Neno, Yeye alikuwa ndiye thibitisho la ahadi Yake. Yesu, akizungumza na huyu Kleopa na rafiki yake, njiani wakienda Emau, ilikuwa ni thibitisho la Neno Lake lililoahidiwa, na hata hivyo hawakulielewa.

38 Na hebu niliseme leo. Baada ya miaka elfu mbili ya mafundisho, kuamini, Yeye angali hai, nao watu hawawezi kufahamu hilo. Hawawezi kulielewa. Jambo kuu ni kwamba wamejazwa kasumba na mambo mengine sana, shughuli nyingi kupita kiasi, na mambo mengine kupita kiasi. Hiyo ndiyo sababu hawawezi kulielewa.

Walikuwa wamehuzunika sana na kuvunjika moyo, kujua hilo.

39 Sasa, angalia, walikuwa wakizungumza kumhusu Yeye. Sasa walikuwa njiani wakielekea Emau, walikuwa wanaenda kurudia kazi yao ya kale tena. Naye Petro alienda kuvua samaki, na baadhi ya wale wengine wakaenda pamoja naye. Naye Kleopa na rafiki yake, wakasema, "Vema, tutaenda huko Emau." Huko ndiko labda walikoishi, na yapata mwendo wa Sabato, maili chache upande wa pili wa kilima.

40 Na asubuhi hii nzuri ya Pasaka, Yesu amefufuka kutoka kwa wafu! Amefufuka! Neno Lake, Neno la Mungu, lilikuwa limetimia. "Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitamwacha nanii Wangu. . .sita—sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu," lilikuwa ndilo Neno. Angalia, Daudi alilinena.

41 Yesu alisema, "Liharibuni hekalu hili, nami natalijenga tena katika siku tatu." Mnaona? "Mwana wa Adamu anapanda kwenda Yerusalemu, kuwekwa mikononi mwa Mataifa, na watu katili, kudhihakiwa na kupigwa mijeledi, na kusulubishwa, bali katika siku ya tatu atafufuka tena." Alisema hivyo, hili lilifaa kumaliza yote.

42 Na hapa hawa watu aliowaambia hilo, waliolifahamu Neno, wakitembea barabarani, wamehuzunika kuhusu jambo hilo. Unaweza kuwazia kioja kama hicho? Bali kwa hakika kimejirudia tena. Kimejirudia tena.

43 Tunaona, walipokuwa wakitembea barabarani, jambo moja kuu kuwahusu, walikuwa wakizungumza juu Yake hapo alipojitokeza.

44 Sasa hiyo ndiyo shida leo hii, sababu nafikiri Yeye hawatokei wengi wetu, ni kwa sababu hatuzungumzi kumhusu Yeye vya kutosha. Tunayo mambo mengine yanayotubidi kuzungumzia. Tofauti zetu za kimadhehebu, inatubidi kuzozania hizo. Inatubidi kuzungumzia ukomunisti. Tuna kila namna ya mipango, na kila kitu kingine, yote yametufunga. Hatuna muda wa kuzungumza kumhusu Yeye. Mpango wa kanisa, ni nani atakayekuwa mchungaji mchaguliwa, ni nani atakayefanya *hili*, na ni nani atakayefanya *lile*, tunazungumza kuhusu kila kitu kingine isipokuwa Yeye.

45 Wakati, tunapaswa kuwa tukizungumza kumhusu Yeye! Hivyo daima. Hilo linapaswa kuwa ninii ye—yetu. . .Hilo linapaswa kuwa kusudi letu, hilo linapaswa kuwa ma—maisha yetu yote, ni katika Yeye.

46 Nilimwambia mtu fulani hivi majuzi. Alisema, "Mbona, unaamini mambo hayo?"

47 Nikasema, "Bwana, nilitumia maisha yangu. Hiyo ni kweli. Ningetoa maisha yangu kwa ajili ya Hilo. Laiti ningalikuwa na maisha elfu kumi ya kutoa kwa ajili Yake. Ningali ninaliamini."

48 Hakika, inatubidi kuwa tukizungumza kumhusu, ikiwa tunataka kumwona Yeye. Hapo ndipo, daima.

49 Walipaswa kumtambua, bali hawakumtambua. Alipotembea kando yao, walipaswa kumtambua. Kumbukeni, walikuwa wametembea na Yeye kwa miaka mitatu. Na hapa ninii. . .Je! ungeweza kuwazia? Wanafunzi Wake waliokuwa wametembea Naye kwa miaka mitatu, Yeye hapa anatembea moja kwa moja kando yao, nao ni vipofu tu kama popo. Kwa nini? Kwa

sababu hawakujua Maandiko. Na, hata hivyo, Yeye alikuwa amewaambia Maandiko.

50 Naye huyu hapa, *Imanueli*, "amefanyika mwili, akakaa katikati yetu," nao Mafarisayo hawakutambua hilo. Wasingeweza kuelewa hilo, jinsi Mtu huyu . . . Vema, walimsulubisha, kwa sababu, alisema, "Aliivunja Sabato na—na kujifanya Mwenyewe Mungu." Hiyo ndiyo sababu walimsulubisha. Sasa tunaona, kwamba sababu ya wao kukosa kujua hilo, ni kwa kuwa hawakuyajua Maandiko.

51 Sasa wanafunzi hawa walipaswa kumtambua, bali hawakuyafahamu Maandiko. Hapa basi akawafunulia, angalia, alivyoanza kutembea, aliwafunulia ahadi za Maandiko kumhusu Yeye kwa ajili ya wakati huo; si ahadi za Maandiko katika wakati wa Nuhu, si ahadi za Maandiko kwa ajili ya nyakati zingine. Ahadi ya Maandiko kumhusu Yeye Mwenyewe kwa ajili ya wakati huo, hiyo ilionyesha hakika kwamba Yeye ni nani. Mnaona?

Alianza kuwauliza, kasema, "Kwa nini mmehuzunika sana?"

52 "Kwa nini," wakasema, "je! Wewe ni mgeni hapa?" Wakimkazia macho. "Je! Wewe ni mgeni hapa, hata huyajui mambo yaliyotokea? Mbona, Yesu wa Nazareti, nabii aliyethibitishwa na Mungu, nasi tulitumaini kwamba Yeye angekuwa Ndiye angeikomboa Israeli; na leo ni siku ya tatu, nao wamemsulubisha, na mambo haya yote." Naye akaninii tu . . .

53 Akasema, "Ni mambo gani yaliyotokea?" Kana kwamba hakujua lolote kuhusu hayo. Mnaona, Yeye alifanya tu kana kwamba Yeye—Yeye hakujua chochote kuhusu hayo.

54 Bali sasa kumbukeni, wakati Yeye alipoanza kuzungumza basi, alianza kuwafunulia ahadi zilizomhusu Yeye Mwenyewe. Kasema, "Hamjui jinsi inavyompasa Kristo kupitia mambo haya na kuingia katika utukufu Wake?" Ndipo basi akaanza, kwa Maandiko, kuanzia Musa na manabii wote, na kuwafunulia Maandiko yaliyomhusu Mwenyewe, Masihi. Kile Masihi alichopaswa kuwa, matendo yale yalimpasa kutenda, kila kitu ambacho hana budi kuwa, Yeye aliwafunulia hayo, na wangali hawakumwelewa.

55 Kama hayo siyo marudio, leo hii! Yeye anafanya jambo lile lile, na kanisa lingali linatangatanga gizani. Akiwafunulia kuwa Yeye ni Nani na kile alicho, na—na wangali wanasema, "Vema, sasa, ninaamini kanisa langu hufundisha . . . " Haya basi. Mnaona, hiyo ndiyo sababu nyinyi . . .

56 Rudini kwenye Maandiko, yachunguzeni Maandiko, Hayo yana Ukweli. Tumeyapindua sana Hayo. "Tunajuaje kwamba ni Maandiko?" Wakati yanapokuwa ni Maandiko yaliyoahidiwa kwa ajili ya wakati huo.

57 Sasa, Yeye hakurudi nyuma na kusema, “Mnamkumbuka Musa, yale aliyofanya?” Mnaona? Yeye aliwafunulia Maandiko yaliyomhusu Yeye, kwa ajili ya wakati huo. Yeye alikuwa ndiye Nuru ya wakati huo.

58 Musa alikuwa ndiye nuru ya wakati wake. Yeremia alikuwa ndiye nuru ya wakati wake. Ilikuwa ni nuru ya Mungu ikiangaza kwa ajili ya Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo. Kila wakati una Neno lake lililoahidiwa. Mungu huwatuma manabii Wake na kulifunua Neno hilo; humthibitisha nabii Wake, kwanza, halafu analifunua Neno hilo na kulifanya liishi.

59 Naye Yesu alikuwa ndiye Kristo. Na kila kitu kilichomhusu Kristo, alikuwa amekithibitisha. Kuzaliwa na bikira, aliwaponya wagonjwa, akatambua mawazo yaliyokuwa mioyoni mwao, kila kitu alichopaswa kufanya ili kuwa Ma—Masihi, na, hata hivyo, alifufuka kutoka kwa wafu, na wangali hawakulitambua. Wangali hawakulijua. Baada ya Maandiko kufunuliwa, wangali hawakumtambua Yeye, ingawa Yeye alikuwa ni lile Neno lililoahidiwa. Sasa kumbukeni jinsi hilo lilivyo la kupendeza, Neno ambalo alikuwa akiwafunulia, akiwaonyesha. Walikuwa wametembea na Yeye moja kwa moja kwa miaka mitatu, na kutambua hilo, wakajua kwamba Yeye alilitimiza Neno hilo. Hao hapo wakaenda, wakitembea kuelekea huko Emau, “Ndivyo ilivyo?” Aha! Hawakulielewa kabisa! Hawakulifahamu.

60 Angalia basi ilipofikia mahali, baada ya Yeye kulifunua Neno, tena, kwao, na kuwaonyesha jinsi Kristo hana budi kufanya mambo haya, na bado hawakulielewa. Angalia karipio walilopata, hao wahubiri, kwa kutofahamu wala kutambua Maandiko yaliyotimia ambayo yalitimizwa machoni pao. Angalieni maneno Yake kwao, “Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini.” Hapa alikuwa ni Mungu Mwenyewe, Masihi aliyefufuka, akitembea pamoja nao, akiwaonyesha. Kasema, “Mbona, kwani hamwelewi ya kwamba Kristo hana budi kufanya mambo haya? Hivi hamjui kwamba sharti iwe namna *hii*, na namna *hii*, na *hivi* na *hivi*?”

61 Na siku nzima, akiwaeleza katika Maandiko, na hata hivyo, “Ndivyo ilivyo?” Wala hawakujua kwamba alikuwa ni Yeye akisimama papo hapo.

62 Ndipo akaangalia kote. Baada ya kulihubiri Neno, na alikuwa amewaambia na kuwaonyesha mambo yaliyopaswa kuwa, na wangali hawakufahamu hayo. Akasema, “Enyi msiofahamu, na wenye mioyo mizito kuelewa, mnaona, kuelewa Maandiko yaliyothibitishwa ya wakati huo,” Maandiko yaliyomhusu Yeye katika siku hiyo. Hata hivyo alikuwa na wanafunzi, bali hawakujua Neno lililoandikwa walipoliona likidhihirishwa.

63 Ninataka kuacha hilo lizame, muda mfupi tu. Mnaona? Mnaona, hawakujua wakati ninii . . . Unaisoma kutoka kwenye Maandiko, kwamba ni ahadi kwa ajili ya siku hii, na halafu unamwona Mungu akiidhihirisha, na ungali unasema, "Sijui." Ni kitu kile kile, unaona, hakika. Tungali tunahusika na wanadamu.

64 Basi tunaona kwamba aliwakemea, vikali. Walikuwa ni wanafunzi. Kwa sababu, hawakujua Neno, kwamba, Hilo lilipofanyika mwili machoni pao, hawakulifahamu.

65 Nini? Jambo lile lile limetokea leo hii. Bali katika nia za watu . . . Inakufanya uwahurumie, kwa sababu mmoja analo kundi linaelekea *huku*, na mwingine ana lingine linaenda *huku*, na yote wanayowaza ni kuhusu kulifanya kundi hilo likue. Hiyo ndiyo sababu kwamba Kristo hawezi kujifunua Mwenyewe kwa watu.

66 Mbona, kanisa linapaswa kuwa ndilo ninii sana . . . Mbona, linapaswa kuwa katika hatua yake tukufu sasa, na nguvu za kufufuka Kwake, ishara kuu na maajabu.

67 Badala ya hayo, wamechezacheza sana na hili, mpaka wanaingia kipofu katika Baraza la Ekumeni, kuitwaa alama ya mnyama, nao hawajui; hiyo ni kweli kabisa, wakijua Neno Lake linasema kwamba lingefanya hivyo. Nao wanafikiri ni jema kabisa, ni la kupendeza, linatoa pendekezo zuri, na kwa hiyo watalifanya. Wawili wanawezaje kutembea pamoja? Nyinyi Wapentekoste mnaenda kufanya nini? Itawabidi kuachilia mafundisho yenu ya kimsingi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, kufanya hivyo. Hakika, mtafanya hivyo. Haya basi. Mtafanya nini wakati huo ukiwadia? Kuingia tu moja kwa moja katika hilo kijinga!

68 Baadhi ya viongozi wa watu wa Pentekoste, watu wa full Gospel, husimama katika mabaraza haya, na kuketi mbele ya Vatikani, na kundi la maaskofu, na kadhalika, na kusema, "Ndiyo hisia ya kiroho kuliko zote."

69 Mtu aliyekufa ganzi namna hiyo kwa Roho wa Mungu, ambaye angesababisha hali kama hiyo, si ajabu Yeye angesema, "Enyi msiofahamu, na wenye mioyo mizito kuamini yale Maandiko yaliyosema." Yeye angenena usiku wa leo, kama alikuwa akizungumza kupitia chombo, angesema jambo lile lile. "Enyi msiofahamu, na wenye mioyo mizito kuamini jinsi ambavyo wakati Neno limedhihirishwa papa hapa, na halafu mnaingia moja kwa moja ndani yake." Vivyo hivyo sasa!

70 Tunajishughulisha sana na mipango yetu. Sana . . . Walikuwa wamechukuliwa sana, kumsikiliza Yeye, na kufanya mambo mengine. Na—na kwa hiyo tunaona, kwamba, sasa tuna kanuni nyingi sana mbali mbali za imani, tuna vipindi vingi sana vya televisheni.

71 Na sasa tuna harakati ya kupinga ukomunisti. Nilikuwa nikisikiliza *Life Line*, hivi majuzi asubuhi, wakitoa ushahidi ulioandikwa kuuhusu, kwamba—kwamba, ukomunisti, mbona, usingeweza kuufutilia mbali. Mbona, wamekuwa humu ndani kwa miaka na miaka na miaka. Mipango hii yote mbali mbali na mifumo, ilivyosema *Life Line*, hata kwenye kampeni hizi kama zenye ugonjwa wa kupooza, na vitu kama hivyo ndani yake, katika harakati ya kupinga ukomunisti. Harakati ya kupinga ukomunisti, wakomunisti wako hapo ndani wakiutia msukumo, ili tu kuona nani ndiye nani. Loo, jamani! Sina haja na huo.

72 Nina haja na Kuja kwa Yesu Kristo, kwa ajili ya Kanisa. Wahudumu wanapaswa kujishughulisha kuhusu hilo, na kuona kile Maandiko yaliyoahidi leo hii. Sitazamii kuchukua mamlaka, kwa wakomunisti. Ninatazamia Ufalme ujao, Yesu Kristo, na Utawala wa Miaka Elfu kuingia. Hata (kabisa) sina haja na ukomunisti wala mifumo yao, au itikadi zenu za kidini, si hata moja ya hizo! Nina haja na Yesu Kristo, na Yeye pekee, kuwafanya watu wamwone. Yeye yupo hapa, akijithibitisha Mwenyewe, hapa akionyesha hasa kile Yeye alisema kuwa angefanya katika siku za mwisho.

Sasa hawakulielewa. Walichukuliwa sana na shughuli.

73 Hata hivyo, wanadai kuamini leo kwamba alifufuka kutoka kwa wafu. Kila mtu, unaamini alifufuka kutoka kwa wafu? Wale ambao kweli wanadai kuwa ni Wakristo, wanaamini hilo. Halafu basi Yeye anaweza kuja moja kwa moja karibu na kufanya hasa kile Yeye alichosema angefanya baada ya kufufuka Kwake, na wangali hawakioni. Naam, bwana. Loo! Ni kweli. Hao, hao bado hawakioni.

74 Kanuni za imani, mifumo ya elimu, wamewapeleka wahudumu wao huko na kuwaelimisha sana. Itapofusha, ni vipofu kwa theolojia zao za kujibunia, kwamba wako nje ya Neno la Mungu.

75 Kama nilivyosema jana usiku, Mungu hahitaji mfasiri yeyote. Siwezi kulifasiri Neno Lake, wala mtu yeyote kufasiri Neno Lake. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Wakati aliposema kuwa angefanya lolote, Yeye analifanya, na hilo latosha. Ni hayo tu. Alisema angelifanya, Naye akalifanya. Hilo latosha. Hamhitaji mtu yeyote kusema *hili ni* Lile, ama *hilo ni* Lile. Yeye hulifanya, Mwenyewe. Fasiri zetu si kitu kwa Maandiko. Yeye hunena, Mwenyewe, na hivyo ndivyo lilivyo.

76 Wakati wa mwanzo, Yeye aliposema, “Iwe nuru,” na ikawa nuru. Hiyo haihitaji fasiri yoyote. “Bikira atachukua mimba,” alichukua! “Nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili,” akafanya hivyo. Haihitaji fasiri yoyote.

77 Lile alilosema kuwa angefanya katika siku hii, Yeye amelifanya. Halihitaji kufasiriwa; hujifasiri lenyewe. Yeye Ndiye anayejifasiria Mwenyewe.

78 Sasa, bali tumechukuliwa sana na mambo mengine, na tumewapeleka watu wetu kando. Na nyingi za misheni zetu za full Gospel, na kadhalika, na shule, humpa mtu jaribio la akili kabla . . . jaribio la akili, mbele za mwa—mwanasaikolojia, kabla hajaweza ku—kuwa mmishenari, kuona kama IQ yake ni ya juu vya kutosha. Hilo si ni jambo fulani? Ningeweza kuwazia hilo katika kitu fulani baridi, kitu fulani cha mbali kilichokufa miaka mingi iliyopita. Lakini kitu kipya kama Pentekoste ilivyo, wangewezaje kufanya jambo kama hilo?

79 Hivi uliwazia IQ waliyohitaji kwenye Siku ya Pentekoste? Imani katika Mungu, hiyo ndiyo waliyohitaji. Kweli! Hiyo ndiyo inayohitajika. "Ikiwa unaamini, ishara hizi zitafuatana na hao waminio," Yesu alisema. Kamwe hakusema wapimeni IQ yao. Yeye alisema, "Nendeni ulimwenguni kote," wamishenari, "mfanye wanafunzi kutoka mataifa yote. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio!" Hiyo ndiyo IQ, IQ ya Mungu, kama una imani ya kutosha kufanya mambo haya kuwa hai na halisi, Kristo akidhihirishwa kwa watu.

80 Lakini, leo hii, tunataka kuwapima na namna fulani ya mfumo wa elimu. Jamani!

81 Kumpima Jack Ruby, hivi majuzi, kwa kichaa. Wangali wanafanya hivyo. Ulimwengu wote una kichaa. Hakika, mtu huyo ana kichaa. Hakuna mtu angaliweza kumpiga mwenzake risasi kama hana kichaa. Ulimwengu wote una kichaa. Hakika, una kichaa. Mkulima, ana kichaa kwa mfanyabiashara. Mfanyabiashara ana kichaa, kwa mkulima. Ni nani aliye na kichaa? Kundi lote lina kichaa.

82 Lipo jambo moja tu timamu, na hilo ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu, nayo Injili Yake ina jibu kwa kila jambo. Vitabu vyetu vya saikolojia, na mambo haya yote, ni upuuzi. Kama ni kinyume na Neno hili, litupilie mbali. Neno la Mungu ni sahihi, na mengine yote si sahihi.

83 Tunaona mambo haya. Si ajabu ulimwengu umeloweshwa damu! Si ajabu mambo yako jinsi yalivyo sasa! Hatuninii . . . Ni kila wakati tu . . . Nashangaa kama Oswald, aliyemwua Rais wetu, nashangaa kama angalipata kupimwa kichaa. Ninatilia hilo shaka. Bali, unaona, mtu anawezaje kuingia mbio na kumpiga mtu mwingine risasi, halafu amwue na kuendelea? Sasa, niko Texas, nitakoma tu kwa hilo. Bali hebu niwaambie jambo fulani, kamwe . . . Bwana atalishughulikia lote, siku moja, katika Kuja Kwake. Angalia, huna haki yoyote kuutoa uhai wa mtu yeyote. La, bwana. Mungu ndiye pekee aliye na haki kuutwaa uhai. Ni kweli.

84 Sasa angalieni, Neno limeandikwa kwa kweli, ahadi kwa ajili ya wakati huo, likathibitishwa kikamilifu, na wao wangali hawakutambua Hilo. Angalieni, walikuwa tu wamemtambua kuwa ni nabii, Yesu wa Nazareti. "Je! Wewe pekee ni . . .

Je! Wewe ni mgeni hapa? Yesu wa Nazareti, aliyekuwa nabii mwenye uwezo katika kutenda mbele za Mungu na watu." Walimtambua kuwa nabii! Basi, kama walikuwa wamemtambua kuwa nabii, nabii anatumwa kwa wakati huo anaoishi. Anapaswa kudhihirisha ahadi ya Mungu. Neno humjia nabii. Na kama alikuwa ndiye nabii, basi Neno lililoahidiwa la wakati huo lilipaswa kudhihirishwa na Yeye, na bado hawakumwona. Kamwe wasingeweza kuona hilo.

85 Wakasema, "Alikuwa nabii, mwenye uwezo katika kutenda," na zilizokuwa kazi Zake, "mwenye uwezo katika Neno mbele za Mungu, na kadhalika. Alikuwa mwenye uwezo sana, nasi tulitumaini. . . " Israeli waliweka matumaini yao juu Yake; Israeli ya kiroho, si Israeli kanisa, ninii. . . taifa tu. Wa—watu, Israeli halisi ya kiroho walijenga matumaini yao juu Yake.

86 Na, angalieni, basi wakati walipomtambua kuwa nabii, Yeye aliendea kitu gani? Alifanya hasa kile nabii anachopaswa kufanya, alirudi moja kwa moja kwenye Neno. Mnaona? Kurudi moja kwa moja, kuonyesha. Kama alikuwa ni nabii yule waliyesema alikuwa, anarudi nyuma moja kwa moja kuonyesha Neno lililoahidiwa kumhusu Yeye Mwenyewe, la siku hiyo. Wangali hawakumtambua. Akatembea moja kwa moja, vipofu walivyoweza kuwa, hawakutambua hilo. Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku yao, alikuwa ndiye nabii wa kudhihirisha jambo lilo hilo.

87 Sasa angalia, Yeye alisema, "Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito kuamini yote waliyosema manabii kumhusu Kristo, jinsi ambavyo hana budi kupitia mambo haya ambayo Yeye alisema, na ndipo aingie katika utukufu Wake, na kufufuka siku ya tatu. Haya yote anapaswa kuyatimiza, na hata hivyo nyinyi hamfahamu?" Walipaswa wawe wanajua kwamba kulikuwako na Mtu aliyekuwa akifanya thibitisho la yale waliyokuwa wakisema kuwa waliamini. Bali wangali hawakuweza kuliona. Yeye hakika alikuwa ni ishara ya kweli ya na—nabii wa kweli, daima; kutorudi nyuma kwa neno jingine, huko nyuma kwa jingine, bali kuthibitisha Neno kwamba leo hii Yeye yuaishi katika ahadi Yake.

88 Sasa kumbukeni, kabla ya Yeye kuja, Yohana alikuja jukwaani. Alikuwa ni nabii. Na yeye alikuwa ni nini? Mtangulizi wa Masihi. Naye alisema, "Mimi siye Masihi." Walidhani alikuwa, kwa sababu alikuwa nabii. Akasema, "Mimi siye Masihi. Sistahili hata kuvifungua viatu Vyake, lakini Yeye amesimama miongoni mwenu." Loo, Yohana alikuwa na hakika Yeye alikuwa pale, maana alijua ilimpasa kumtambulisha.

89 Baba yake alikuwa ni kuhani. Hakuenda kwenye seminari yao, kujifunza kuwa kuhani. Kazi yake ilikuwa muhimu zaidi. Alienda nyikani, kuwa peke yake na Mungu. Hakutaka kubeba kadi ya ushirika kutoka kwa mtu yeyote, ama wangesema *hili*,

*lile*, au *linginelo*, maana wangechanganyikiwa na kushawishiwa na—na utaratibu wa mwanadamu wa siku hiyo. Kazi yake ilikuwa muhimu. Ilimbidi kumtegemea Mungu pekee, kwa kuwa alikuwa amtangaze Masihi.

90 Yesu alisema, "Alikuwa ni mwanga mkuu uliong'aa, na kwa muda mlitamani kutembea pamoja naye, mlifurahia kutembea karibu naye. Bali ninao ushuhuda mkuu kuliko wa Yohana." Mnaona? Yeye ni . . . Wangali hawakuamini hilo.

91 Ishara halisi ya nabii wa kweli, akipaa juu, kuwarudisha kwenye Neno. Wasingeweza kuelewa namna ya maongezi Yake.

92 Na, tazameni, Maandiko yalikuwa yamesema hilo lilikuwa linaenda kutukia, hasa neno kwa neno jinsi lilivyokuwa. Hata Daudi, mamia ya miaka kabla ya hapo, yapata miaka mia nane, alilia kitu kile kile alichosema msalabani. Na hapana shaka, kwamba katika hekalu asubuhi hiyo, huenda waliimba wimbo uo huo, Zaburi 22, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Hekaluni wakiimba juu yake, na, Mungu yeye yule waliyedai kumtumikia, walikuwa wanamsulubisha.

93 Ndivyo ilivyo leo hii! Mungu yule wanayedai kuwa wanamwamini, anayejidhihirisha Mwenyewe, wataninii, mtafunga kila mlango, na hakuna ushirikiano, hakuna chochote kingine. Wao . . . Ni kinyume na kanuni zao za imani. Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito kutambua siku tunayoishi! Si Mungu ameahidi haya katika siku za mwisho? Jinsi ambavyo kanisa hili la Laodikia lingekuwa vuguvugu, na Yesu akiwa nje, akijaribu kuingia apate ushirikiano mdogo? Yesu ni nini? Neno, Neno la kweli lililodhihirishwa. Akiwa nje, akijaribu kuingia ndani, na asingeweza kuingia.

94 Saa tunayoishi, hakika, vipofu, namna ile ile. Yesu alisema wangekuwa hivyo. Manabii walisema wangekuwa namna hiyo. "Wenye kiburi, wenye kujisifu, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu. Wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiotosheka, wasiowapenda walio wema, wakiwa na mfano wa utauwa, huku wakikana Nguvu zake," Nguvu za kufufuka Kwake, dhihirisho Lake kwamba Yeye ni yule jana, leo, na hata milele. Na Yeye anaishi leo, hata milele, kuthibitisha mambo ambayo Yeye alisema. Siwapigii makelele, bali ninawatakeni kusikia.

95 Kweli, macho yao yalikuwa yangali yamefumbwa. Angalieni, ingawa hawakuweza kuamini, kulikuwa na kitu fulani ndani yao, walimwalika aingie ndani. Alijifanya kana kwamba alikuwa anaenda kupita.

96 Huenda akajifanya hivyo kwako, usiku wa leo. Sasa katika kufunga, ninaenda kufunga mapema kusudi niweze kuwa na mstari wa maombi. Huenda akajifanya kana kwamba anaenda kukupita. Huenda kadi yako ya maombi haitaitwa, bali, kumbuka, labda anakupa tu jaribio, pia. Unaona, Yeye ni Mungu

tu huko nje sawa na alivyo hapa juu, ama popote pale. Yeye huthibitisha hilo, siku baada ya siku, usiku baada ya usiku. Yeye ni Mungu, kila mahali. Unaona? Yeye yuko kila mahali.

97 Sasa kumbukeni, Yeye hujifanya kana kwamba anaenda kupita. Nao wakamshawishi. Sasa, hawakuelewa kile Yeye alichokuwa akizungumzia, lakini hata hivyo mioyo yao yote... Hawakujua cha kuamini.

98 Sasa wapo watu wengi kama hao, leo hii. Wapo watu wengi kama hao katika Beaumont, usiku wa leo. Hawajui kitu cha kuamini. Lakini unajua walichofanya? Walifanya kitu cha busara kuliko vyote mtu yeyote awezacho kufanya, walimwalika aingie ndani. Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Ni hapo, na hapo pekee, awezapo kujifunua Mwenyewe, wakati anapoalikwa kuingia ndani. Mkaribishe ndani, useme, "Bwana Yesu, ninajua Maandiko yanasema hayo. Huenda nisilielewe, bali njoo ndani ya moyo wangu. Ninataka kukukubali Wewe. Ninataka kukuamini. Basi, jidhihirishe Mwenyewe kwangu."

99 Angalia, walimkaribisha ndani. Sasa hawakuweza kulieleza, wao—wao, ni...Yeye, Yeye alininii tu...Hawakuelewa kile alichokuwa akizungumzia. Chote kilikuwa kinatatanisha, kwao. Wasingeweza kukielewa, lakini hata hivyo walisema, walimwalika, walimshawishi, "Sharti uingie ndani!"

Yeye akasema, "Hapana, i—inanibidi kuendelea."

100 "Loo, lakini, Bwana, Wewe—Wewe lazima uingie ndani! Wewe, Wewe lazima uingie ndani!" Nao wakamshawishi mpaka, wakamwita, na mpaka ilimbidi kuingia ndani.

101 Hivyo ndivyo unavyofanya. Halafu basi akiingia ndani, hapo ndipo Yeye anaweza kujifunua Mwenyewe. Anaweza kujitambulisha Mwenyewe akiwa ndani.

102 Angalia jinsi alivyofanya hilo baada ya kufufuka Kwake. Neno la kweli lililoahidiwa, unaona, hawakutambua kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Bali mara alipoingia ndani yao, ndipo alipoyafumbua macho yao. Kwa njia hiyo, Yeye alipoingia ndani ya jengo pamoja nao pale, aliyafumbua macho yao mara Yeye alipoingia ndani. Aliyafumbua macho yao. Kitu gani? Si kwa kuinua mkono Wake na kusema, "Fumbua, hebu macho yenu yafumbuke." Macho yao yalifumbuka, kwa vyovyote vile, kimwili.

103 Kama huko chini Dathani, au—au Dothani, hasa, palikuwa, huko chini walipokuwa na...Eliya alikuwa huko chini. Nao Wa—Washami walikuwa wamewazingira, ndipo Gehazi akalia, "Baba yangu, Washami wako kila mahali!"

104 Ndipo Elisha akajitokeza pale na kusema, "Walio pamoja nasi ni wengi kuliko walio pamoja nao." Kasema, "Bwana, mfumbue macho mvulana huyo." Na kuzunguka maskini nabii

huyo, na kwenye kilima, kulikuwako magari ya Moto na Malaika wa Moto.

105 Na Biblia ilisema, "Aliwapiga kwa upofu Washami." Alijitokeza huko nje na kusema, "Je! mnamtafuta Eliya?"

Wakasema, "Naam, tunamtafuta."

106 "Njoni, nitawaonyesha mahali alipo." Nao wangeweza kuona, kimwili, akitembea moja kwa moja akiteremka. Bali walikuwa vipofu kujua kuwa alikuwa ni nani.

107 Na hiyo ni, usiku wa leo, huenda ukawa na uwezo wa kuona wa ishirini-ishirini kwenye macho yako. Bali, roho yako, je! waweza kufahamu kwamba ni Neno lililoahidiwa la siku hii? Ni ahadi ya Mungu. Mungu aingie ndani, kisha ayafumbue macho yako. "Loo, huyo ni Yeye, sivyo?" Aliliahidi. Angalia, ndani, Yeye aliyafumbua macho yao kujua kuwa Yeye alikuwa ni Nani, alikuwa ni Nani. Sasa iwapo anaweza kuingia ndani yako, usiku wa leo, kwenye mkondo wako wa imani, Yeye anaweza kuyafumbua macho yako, kukuonyesha Waebrania 13:8 ni kweli, kwamba, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kama anaweza kuingia ndani na kufumbua macho yako, Yeye atafanya vivyo hivyo sasa.

108 Kama tu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, tuliyemzungumzia jana usiku. Sasa angalieni, yeye alijua, kwa Maandiko, kile Yeye alipaswa kuwa. Sasa, huo ulikuwa ndio upande mzuri kumhusu mwanamke huyo.

109 Wengi wetu, leo hii, hawajui, kwa Maandiko, kile Yeye alicho leo hii. Tunamweka kwenye hori, kila Krismasi. Naam, tunachukua sungura wa Pasaka na kumfanya ufufuo Wake. Si ajabu tumechanganyikiwa kabisa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Si ajabu hatujui mahali tulipo. Bali mwanamke huyu alijua, alikuwa niani mwake, ndani ya moyo wake kulikuwa na ile Mbegu.

Kama nilivyoichora, kwa rafiki yangu msiri, Jack Moore, leo hii.

110 Jinsi ambavyo wale Mafarisayo kwenye upande wa giza *hapa*, mioyo yao ilikuwa na giza huko nyuma. Hawakuwa na Uzima, kwa kuanzia. Walipoanza kupata nuru kidogo, walipanda juu, kwa sababu walikuwa wa kidini na walisaidia kuziweka amri. Ndipo wakati Neno, huko nyuma katika mwanzo, ilikuwa ikiangazia kupitia Neno, Biblia, kwao; walikuwa wakitembea, bali *huko* nyuma hawakuwa na Nuru.

111 Hapa alikuwepo maskini huyu, kahaba mwenye sifa mbaya, maisha yake ya kwanza *hapa* juu yalikuwa na giza kabisa, kutoka kwa maisha yake. Alikuwa ni kahaba. Pili, chini, kulikuwa na Nuru kidogo tu, kwa kuwa alikuwa na dhana ya kile Masihi angekuwa.

Hapa alisimama Yesu, katikati yao.

112 Alipoifanya ishara ya Masihi, akawaonyesha kuwa Yeye ni Nani na kila kitu, kilitia giza kabisa kitu chote cha Mafarisayo. Walirudi nyuma kwenye giza. Hawakuwa na chochote *hapa* chini cha kushikilia. Walimwita "Beelzebuli," pepo. Na ile nuru waliyokuwa nayo, ikazimika, nao wakaangamia katika hiyo.

113 Hapa alikuwapo mwanamke huyu, mwenye giza ya dhambi alivyoweza kuwa, bali ndani ya moyo wake alijua kile huyo Masihi angekuwa. Alijua ni ishara gani Yeye angeonyesha. Na mara tu alipomwambia . . .

114 Alisema, "Nipe maji ninywe." Mwanamke akasema . . . Yeye alikuwa akiwasiliana na roho yake, kuona msimamo wake.

Naye akasema, "Si desturi."

115 Yeye akasema, "Kama ungalijua ni Nani unayezungumza naye, ungeniomba Mimi maji." Ndipo mazungumzo yakaendelea. Moja kwa moja alipata mahali hasa mawazo yake yalipokuwa, na kilichokuwa moyoni mwake.

116 Mwanamke huyo alijua papo hapo kwamba, ajapo Masihi, Masihi ilibidi awe ni Mungu. Mungu ni Neno. Neno huyatambua mawazo yaliyoko moyoni. Hilo ndilo lililokuwa ndani ya manabii. Mwanamke huyo alijua zaidi ya nusu ya wahubiri Marekani wanavyojua usiku wa leo, hiyo ni kweli, hiyo ni kweli kabisa, na yeye katika wakati—wakati huo. Lakini, unaona, alikusudiwa Nuru, na mara tu Nuru hiyo ilipoangaza!

117 Naye mwanamke huyo alidhania Yeye alikuwa tu ni mtu wa kawaida, labda pendekezo. Akasema, "Mbona, baba zetu waliabudu katika mlima huu. Na Wewe wasema katika Yerusalemu, ukiwa ni Myahudi," na kadhalika, mazungumzo . . .

Akasema, "Nenda kamwite mumeo na mje hapa."

Mwanamke akasema, "Sina mume yeyote."

Kasema, "Umesema kweli. Umekuwa na watano."

118 Tazama! Ile chembe ndogo ya Nuru, ya kujua kuwa Yeye ni Nani, hiyo ilionekana kama ingeweza kuwa ndiyo. "Bwana, naona kuwa Wewe ni nabii. Ninajua, ajapo Masihi, hayo ndiyo atakayofanya."

Akasema, "Mimi Ndiye."

Mwanamke akasema, "Hilo lilitosha!" Unaona?

119 Giza lake lote lilifanywa nuru. Weupe wote wa Mafarisayo ulifanywa giza, kwa kukataa Hilo. Hiyo ndiyo tofauti, kuangaza Nuru kupitia Neno. Mnaona? Kwa sababu jina lake lilikuwa limewekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ya msingi wa dunia, alitambua Hilo sasa hivi. Ilichukua mbegu hiyo ndogo, ilikuwa imelala nyuma ya uchafu huu wa utovu wa adabu na kila kitu namna hiyo, na kuusafisha.

120 Hilo ndilo lililomleta, kuwasafisha wa aina hiyo ambao Baba alikuwa amempa kabla ya msingi wa ulimwengu. Amina.

Ninajisikia kubarikiwa, nikijua hilo kuwa ni Kweli. "Si yule atakaye, wala yeye apigaye mbio; ni Mungu." Amina. Si kiasi kile ulichofanya, au kiasi kile ambacho hukufanya. Hakuna mtu aliyemtafuta Mungu; Mungu alikutafuta.

121 Na wakati Nuru ilipoangaza, hao Mafarisayo walisema, "Loo, huo, nimesikia upuuzi huo hapo kabla. Yeye ni Beelzebuli. Huyo ni mpiga ramli." Ndipo kitu hicho chote kikaingia giza.

122 Naye maskini mwanamke huyu, giza *hapa* juu, na nuru *hapa* chini. Kasema, "Ninajua Masihi ajapo. Ninamtazamia Yeye. Ajapo, Yeye atafanya hayo. Hapana shaka Wewe ni nabii Wake."

Yeye akasema, "La, Mimi Ndiye."

123 Akasema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Si hilo ndilo Neno ambalo hutambua mawazo yaliyoko moyoni? Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Anapaswa kuwa Marekani, akihubiri usiku wa leo, ingawa ninapinga hilo. Huyo mwanamke, anapaswa kuwa hapa akifanya jambo kama hilo, akiwaonyesha baadhi ya jamaa hawa kile alicho Masihi.

124 Angalia, mara akiwa ndani, aliyafumbua macho yao. Halafu, kwa Maandiko, Yeye alijionyesha Mwenyewe. Sasa Yeye aliyafumbua macho yao.

125 Basi wakati mwanamke huyo aliposema hivyo, aliingia. Mwanamke huyo, ninii . . . Ni kitu gani kilichoingia? Ufunuo; Mbegu hii iliyokuwa *hapa* chini, wakati hiyo Nuru ya Mwana ilipoiangazia!

Unaweza kuchukua mbegu na kuizika chini ya jiwe.

126 Niliona, si muda mrefu uliopita, walipokuwa na mbegu za alizeti walizokuwa wameweka kwenye kifurushi kwa karibu miaka elfu nne, huko Misri. Walichukua hiyo mbegu, na baadhi ya hiyo ngano iliyokuwa ghalani, ambayo Yusufu aliweka mle, miaka hiyo yote. Na ilipowekwa ardhini, na jua likaiangazia, iliishi. Chembe hiyo ya uhai ilikaa pale.

127 Loo, ndugu, wakati tulipochaguliwa na Mungu, kabla ya msingi wa dunia, kuwa wana na binti za Mungu! Nuru hiyo ikiiangazia, hakuna dhehebu, hakuna mipaka ya kanisa, hakuna upinzani, hakuna kitu kitakachoikomesha. Itaishi, maana Mungu alisema ingeishi.

128 Waliitambua. Macho yake yakafumbuka, naye akaijua. Aliijua, mara ilipoingia ndani. Aliyajua Maandiko, hiyo ndiyo sababu alimtambua Yeye.

129 Wanafunzi hawa baada ya kufufuka Kwake, hawakujua Maandiko, na hiyo ndiyo sababu hawakumtambua.

130 Na hivyo ndivyo Mafarisayo hawakulijua. Yeye alisema, "Yachunguzeni Maandiko. Mnadhani mna Uzima wa Milele, Mimi . . . Hayo ndiyo yanayowaambia kuwa Mimi ni Nani."

131 Loo, thibitisho la Utu Wake! Ndipo wakati ahadi inapothibitishwa, macho yao yalifumbuka, nao wakamjua.

132 Pia, kitu kile kile kilichofumbua macho, kilifumba macho, pia. Wale waliokidhihaki Hicho, Milele kiliwarudisha mahali walipokuwa hapo mwanzo, mnaona, kiliyafumba macho yao.

133 Macho ya Petro yalifumbuliwa na kitu kile kile. Alikuwa anakitazamia. Macho ya Nathanaeli. Yesu alisema Yeye aliwajua kabla ya msingi wa ulimwengu, kwamba walipaswa kuwa ndio wajumbe hawa.

134 Sasa mbele ya haya yote, katika wakati huu tunaoishi, imeyafanyia nini macho yako? Sasa hilo ndilo swali, si kile iliyoyafanyia yao. Uko upande gani, usiku wa leo? Sasa ni lazima ama uhusishwe na Mafarisayo, au uhusishwe na wanafunzi, ama waaminio. Sasa imekufanyia jambo fulani. Wewe ni—wewe umeinuka tu dhidi Yake. Imefanya jambo fulani. Kama ungalikuwa unaishi siku hiyo, ungefanya nini? Ha—hali yako ya sasa inakutambulisha na nini? Inakuweka wapi? Wazia hilo.

"Vema, kanisa langu . . ." Hayo ndiyo waliyosema Mafarisayo. Unaona?

135 Je! uko tayari kumtambua Yesu Kristo, kupitia Nguvu za kufufuka Kwake? Je! uko tayari kuacha kila kitu na kutembea pamoja Naye? Je! uko tayari kumwamini Yeye, ukipeleka Nuru Yake na Uzima kwa wengine? Imefanya nini? Kama Yeye—kama Yeye anavyofunuliwa katika siku hizi za mwisho, Yeye aliahidi hiyo.

136 Sasa unasema, "Ndugu Branham, Masihi alifunuliwa wakati ule. Ninajua Maandiko yalisema hivyo."

137 Vema, Masihi yuyo huyo ameahidiwa kujifunua Mwenyewe leo hii. Jambo lile lile! Sasa, Waebrania 13:8, sasa sikilizeni, inamtambulisha Yeye kuwa "yeye yule jana, leo, na hata milele." Yohana 14:8 . . . Ilisema kwamba, "Yeye aniaminiye Mimi, mnaona, kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya." Yohana 14, tisa- . . . hapa tunaona, Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo, na utaratibu wa ulimwengu, *kosmos*, hautanijua tena. Watakuwa vipofu kabisa. Hawataniona tena. Ndipo kitambo kidogo nao hawataniona, hata hivyo macho yenu yatafumbuka, kwani nyinyi mtaniona; kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi ukamilifu wa dahari." "Yeye yule jana, leo, na hata milele."

138 Luka 17:28 ilisema. Yesu alisema kwamba, "Katika siku za mwisho, hali ya ulimwengu ingekuwa tu kama ilivyokuwa wakati Wamataifa walipoangamizwa huko Sodoma na Gomora." Si katika wakati wa Nuhu, kama vile gharika (Alitaja upotovu wa maadili ya siku hiyo), bali Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma." Sasa huo ulikuwa ni ulimwengu wa Mataifa ulioangamizwa kwa moto. Mungu aliweka upinde wa

mvua angani, hakuna tena "maji," bali ni moto wakati huu. Sasa ulimwengu wa Mataifa uko tayari kwa maangamizi.

139 Yeye aliahidi kwamba kungekuwako na upotovu mkuu nchini. Kama uliwahi kuona baadhi ya hizo picha, jinsi wanawake wanavyovalia humo ndani, hiyo samawati chini ya macho yao, inaonekana kama wameoza. Angalia kile wanachofanya leo hii! Utovu wa uadilifu, upotovu, loo, baadhi ya vitu vya kuogofya mno, na taifa hili limemezwa katika hayo. Linaongoza ulimwengu mwingine wote katika talaka. Wanawake wetu wamepoteza maadili ya—ya—yao ya kawaida. Wameuvunja uti wa mgongo wa taifa. Na wote, nusu ya vitu katika Marekani vimejengwa juu ya, ni kujuana kimwili; kila kitu, wiski yao, sigara zao, na kila kitu kingine. Nao madaktari wanasema, "Ni sumu. Itakuua." Wanaendelea tu kuivuta, vivyo hivyo tu. Wataivuta, kwa vyovyote vile. Hawana hisia yoyote ya onyo.

140 Nayo Maandiko yanasema wasikate nywele zao, na kadhalika. Nami sizungumzi juu ya hao wanawake wa ulimwengu; hao ni chakula cha mizinga, hata hivyo. Ila ninazungumza kuhusu nyinyi wanawake wa Kipentekoste. Mnajua bora kuliko hiyo. Biblia ilisema kwamba nywele za Samsoni zilimtenga; kuzaliwa Mnadhiri kulimtenga kwa Neno la Mungu. Enyi wanawake, itafanya jambo lile lile kwenu, mtu aliyetengwa. Naye Mnadhiri ametengwa kwa Neno, mbali na mambo ya ulimwengu. Nawe unalihubiri, na kulilia, na kulipigia mayowe, na ukirudi mwaka ujao na ni mbaya kuliko ulipokuwa huko. Hakuna kitu kilichosalia ila Hukumu ya Kiungu ya Mungu, mabomu ya atomiki na makombora na kadhalika, kwa ajili ya ulimwengu wote.

141 Wachekeshaji kwenye televisheni, na kusema, na—na redio na kadhalika, wanapiga mbinja na kuimba, na kufanya mizaha michafu, na kutamka maneno machafu na mambo mabaya ambayo hata hayafai kuruhusiwa, na magazeti na kadhalika yamejazwa kabisa wanawake walio uchi, wazinifu, kila kitu, wakijaribu kuridhisha moyo, kujaribu kukutuliza. Inanikumbusha kuhusu mvulana mdogo akipiga mbinja gizani, akipitia makaburini, akijaribu kujifanya afikirie kuwa si mwoga. Umetishwa kabisa, na unajua hilo. Unajua hukumu inakungojea, na inakuja kwa sababu umemkufuru Roho Mtakatifu, nawe umemkataa Yesu Kristo aliyefufuka. Kweli kabisa. Macho yao yamefumbwa. Hawajui.

142 Sodoma na Gomora. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa huko Sodoma na Gomora." Kama nilivyolirudia kwenu jana usiku, hakujawahi kuwapo na wakati katika historia ambao umekuwa namna hii. Angalia, Lutu . . .

Daima yapo matabaka matatu ya watu.

143 Lutu aliliwakilisha kanisa, la jina tu. Yuko huko Sodoma huko nje, ambapo wanawake walikuwa na mitindo ya kukata nywele zao, na walikuwa na mambo makuu, naye alikuwa ni mmoja wa wazee wa jijini, na mambo makuu namna hiyo, na, "Hebu niepuke nayo." Lakini, kwa kweli, ndani ya moyo wake, iliitesa nafsi yake. Alijua bora zaidi; alikuwa amekuwa na Ibrahimu.

144 Ibrahimu kamwe hakushuka kuingia huko, kwa kuanzia. Alikuwa ndiye mteule ambaye Mungu alimpa ahadi, aliyekuwa akimtazamia mwana ajaye, mwana aliyeahidiwa.

145 Sodoma bado ilikuwa katika shughuli zake. Na, kumbukeni, Malaika hao wawili walienda huko chini kuhubiri.

Mmoja alikaa na Ibrahimu na kundi hilo.

146 Sasa, angalia, walienda huko chini kuhubiri. Pia, kumbukeni, tangu tuwe katika nyakati hizi za kanisa, hakujakuwapo na mtu aliyetumwa kwa kanisa, jina lake linaisha na h-a-m, mpaka sasa. G-r-a-h-a-m, mjumbe wa majira haya, kwa kanisa lililoko Babeli, huko chini Sodoma. Mwinjilisti mashuhuri anafanya kazi kuu kutoka kwa hiyo, pia. Anawakemea, kulia na kushoto. Hawalitilii maanani. Alisema, "Nitakuwa na waongofu elfu thelathini katika majuma sita; nikirudi katika majuma mengine sita, sina hata thelathini."

147 Shida ni nini? Hawaendi popote. Wanatembea wakitafuna chingamu, wakivuta sigara, na kila kitu, kufanya maungamo, ama kile wanachokiita "uamuzi." Hiyo ni sawa kabisa, acha mwinjilisti aiendeleze jinsi Mungu alivyosema iendelezwe.

148 Kwangu mimi, si uamuzi. Ni kuzaliwa! Huna budi kuzaliwa. Una jambo fulani haina budi kutukia.

Sisi hapa, ingawa, hapo, h-a-m.

149 Angalia, hapa juu kwenye kilima, kuna Mmoja aliyebaki na Ibrahimu, lakini hebu angalia namna ya ishara ambayo Yeye alionyesha. Na hilo lilikuwa ninii la Ib-. . . Mungu alikuwa amemwonyesha Ibrahimu ishara baada ya ishara, bali hiyo ilikuwa ndiyo ya mwisho kabla ya mwana aliyeahidiwa kuja; ya mwisho. Mtu huyo, Yeye alionekana kama binadamu. Alikuwa tu ni Mtu wa kawaida, amevikwa; mavumbi kwenye nguo Zake, kasema alikuwa amekuwa safarini, Ibrahimu akamtawadha miguu.

150 Ndipo basi alipoketi pale, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, sasa angalia, Yeye alisema, "Ibrahimu." Siku moja ama mbili hapo kabla, alikuwa ni *Abramu*, naye mke alikuwa *Sara*, S-a-r-a. Sasa yeye ni S-a-r-a-h, "binti mfalme." Yeye si Abramu. *Ibrahimu*, "baba wa mataifa." Ilimbidi kubadilisha jina lake. Angalia, Yeye alisema, "Ibrahimu, yu wapi mkeo, Sarah?"

151 Sasa kumbukeni, yeye alikuwa na miaka mia moja, naye mke alikuwa na tisini. Kasema, "Yuko hemani, nyuma Yako."

152 Akasema, "Nitakuzuru kulingana na ahadi." Mnaona? Na hiyo ni siku ishirini na nane, kwa Sarah.

153 Ndipo Sarah akacheka, tuseme, kifichifichi, kasema, "Mimi, mwanamke mkongwe, niwe na raha na bwana wangu; yeye akiwa ni mkongwe, pia?"

154 Akasema, "Kwa nini Sarah akatilia shaka hilo, akisema moyoni mwake, 'Mambo haya yanawezekanaje?'"

Naye akakana.

Bali Yeye akasema, "Naam, ulisema hivyo."

Yesu alisema, "Kama tu ilivyokuwa . . . "

155 Sasa angalia. Ibrahimu alitambuaje hilo? Sasa, Ibrahimu alimwita, "Elohimu." Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli, wasomaji wa Biblia? Naam, bwana. Elohimu ni Yule ajitoshelezaye kwa yote, yule Muumba mkuu Mwenyewe. Ni kwa nini alimwita Elohimu? Kwa sababu Yeye aliweza kutambua mawazo yaliyokuwako moyoni. Hilo ni Neno. Waebrania 4, ilisema—ilisema, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, lachoma hata kugawanya viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

156 Hivyo ndivyo, manabii, Yesu aliwaita, "miungu." Hivyo ndivyo Yesu alivyojitambulisha Mwenyewe, ndipo mwanamke huyo alijua Yeye alikuwa ni Neno, Yeye angeweza kutambua mawazo. Naye Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, anapofunuliwa Mwana wa Adamu."

157 Limefanyia nini macho yako? Je! anaweza kuingia ndani, usiku wa leo? Ninatumai anaweza. Kumbukeni tu, hebu tuwe tu na kicho na tuamini kwa moyo wetu wote.

158 Yeye aliahidi, kumbukeni, Malaki 4, kutakuja Ujumbe ambao "utarejesha I—Imani ya baba zao tena, kuwarejesha watoto kwa baba zao." Loo, Wapentekoste wenye kukiri, naomba Mungu ayafumbue macho yenu mapofu katika siku hii, mbali na tofauti zenu za kimadhehebu, na kanuni zenu za imani na mambo mnayoshikilia kichoyo na kuzozania, na mumtazame Mwana wa Mungu wakati Yeye yupo hapa. Miaka elfu mbili, Yeye angali hai na miongoni mwetu usiku wa leo, akithibitisha ahadi Yake.

159 Naomba Mungu, usiku wa leo, wakati anapotuleta pamoja kama Yeye alivyowafanyia kule Emau, aifunge milango na kutufunulia kitu. Kumbukeni, sababu ya wao kujua kwamba huyo alikuwa ni Yeye, Yeye alilifanya kama tu alivyolifanya kabla ya kusulubishwa Kwake; ndipo basi akatoweka machoni pao, kuwaondokea. Yeye alilifanya hivyo. Naomba aje usiku wa leo, miongoni mwetu, na ayafumbue macho yetu, kwa kujifunua Mwenyewe kwetu, kwa mambo yale yale aliyofanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, kwa sababu Yeye aliahidi. Ni yeye yule

jana, leo, na hata milele. Naomba Bwana atusaidie kumwona Yeye anavyojitokeza kwetu.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

160 Ni nini madhumuni yangu? Ni nini kusudi langu kuhusiana na madhumuni yangu? Bwana Mungu, siwezi kusema ndiyo au la. Wewe Ndiwe unayehitaji Hili. Ulilihahidi, nami ninaomba ya kwamba Wewe utawafanya watu waone na kuelewa, usiku wa leo. Wajalie, wakati mmoja, Bwana, wafungue mioyo, wazi kabisa, waseme, "Ingia ndani, Bwana, sasa jifunue Mwenyewe kwangu mimi." Pia jalia macho yao yafumbuke basi, kutambua hilo.

161 Naomba kusiwe na mwenye dhambi yeyote atakayesalia katika jengo hili usiku wa leo, asiyeamini. Loo, huenda hapa kuna wale ambao wangekuwa . . . ambao wange—wangechukizwa sana na mimi kuwaita mwenye dhambi. Lakini, Baba, Mungu, Wewe uliwaita Mafarisayo, ambao walikuwa wa kidini na waaminifu wa dini, "pepo" kasema, "nyinyi ni wa baba yenu, ibilisi, na kazi zake mwazifanya," kwa sababu hawakulitambua Neno lililothibitishwa, Masihi. Wangeweza kumwamini Yeye, katika roho; bali akiwa katika mwili, hapana. Na, hata hivyo, Maandiko yao yalisema kwamba Yeye angekuwa ni "Mungu pamoja nasi."

162 Baba, ninaomba, usiku wa leo, ya kwamba Wewe utajalia tena. Je! wapo wowote hapa wanaotaka macho yao yafumbuliwe? Wape dawa ya macho uliyoahidi katika Ufunuo 3, kwenye Wakati wa Laodikia; wanunue dawa, kusudi macho yao yaweze kufumbuliwa usiku wa leo, ili waweze kuitambua saa tunayoishi, na thibitisho la ahadi ya Mungu katika majira haya. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

163 Kadi zipi za maombi? K. Ni wapi tulininii . . . Tulianzia moja, jana usiku, sivyo? [Mtu fulani anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Ila hatuna muda mwingi sana, dakika kumi na tano au ishirini bado. Hebu tuanzie . . . Naye alisambaza kadi za maombi K. Sasa nyinyi shikilieni kadi zenu, tutafikia kila moja ya hizo.

164 Hili, jambo lingine sasa, baada ya kuzungumza . . . Ilikuwa kwamba, yeyote yule aliyenena, walinena. Kumbukeni hilo, ningeingia tu moja kwa moja na kuanzisha mstari wa maombi. Ilikuwa rahisi zaidi. Lakini, leo hii, i—i—inanibidi kufanya jambo tofauti. Mnaona? Na si—sina budi kuleta Hili, hivyo tu. Likipokelewa . . . Ni—ninaweza tu kupanda Mbegu. Si—siwezi kuifanya iishi. Haina budi kuanguka kwenye udongo mzuri.

165 Mwajua, Mbegu Yake Mwenyewe, walisema Yeye alipanda. Zingine zilianguka kando ya njia, hazikufaa kitu hata kidogo. Zingine zilianguka kwenye miiba, bali, na kwenye mawe. Lakini zingine zilienda kwenye udongo mzuri. Huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu.

Ninaweza tu kupanda Mbegu, kwa njia iyo hiyo. Mnaona?

166 Naomba achukue ujinga wangu, auweke upande mmoja; na auchukue moyo wangu, kwamba ninamwamini, na kuangalia chini na aone ikiwa ninampenda Yeye, au sivyo; na kisha anisamehe dhambi zangu zote, na kunitumia kwa njia yoyote ambayo Yeye—Yeye anaweza kujipatia utukufu kutoka kwangu. Uzima au mauti, haijalishi, ili tu kwamba impe Yeye utukufu.

167 Sasa ninaomba kila mtu, katika Jina la Bwana Yesu, tafadhali kaeni kwa dakika chache tu. Msitembee huku na huku. Hii daima itakuwa namna hii. Hivi mnaweza—mnaweza kuwazia matarajio ya kuonekana kwa Yesu Kristo?

168 Sasa kama nilitembea hapa nje, kama mwanadamu, kasema, "Mimi ndimi Bwana Yesu," akiwa na nywele ndefu; hatujui kama alikuwa nazo au sivyo. "Nina makovu ya msumari mikononi mwangu," a-ha, mnafiki yeyote anaweza kufanya hayo. "Ninayo mafuta na damu, na kila..." Hayo, bado, hayo hayana... Maandiko hayakuahidi hayo.

169 Ungemjuaje Yesu? Huninii...Unasema, "Vema, ningemjua kwa picha Yake." Hapana, hiyo ni saikolojia fulani ndiyo iliyochora hiyo. Hatujui alivyoonekana. Mnaona? Sijui kile Yeye alichokuwa. Hiyo ni, mnaona, haina budi kuwa hivyo.

170 Rebeka hakujua sura ya Isaka, bali ilikuwa ni upendo, hata hivyo. Mnaona? Hakujua sura yake; ilimbidi tu kwenda. Mifano! Alimwona akampenda. Alikuwa tayari kwenda, kwa vyovyote vile, haijalishi alivyoonekana.

171 Lakini mimi ningemjuaje? Yesu alisema, "Kwa matunda yao wanajulikana." Sasa kama Yesu angalikuwa hapa, asingalikuwa katika mwili kama nilivyo mimi, maana mwili huo unakaa kwenye mkono wa kuume wa Ukuu, bali Uhai Wake upo hapa.

172 Pia, kumbukeni, hii ndiyo ahadi ya mwisho, ishara ya mwisho ambayo kanisa linapata, kabla ya ishara iliyoahidiwa—Mwana aliyeahidiwa kurudi. Andiko hilo haliwezi kuvunjwa, mwajua. Punde tu baada ya Sodoma, mwana aliyeahidiwa aliwasili, na Sodoma ikateketezwa. Ndivyo itakavyokuwa tena!

173 Hebu tuite kuanzia kadi ya maombi, tuseme yapata... Tulifikia wapi, moja hadi kumi na tano, jana usiku? Hebu tuchukue kumi na tano zingine, themanini na tano hadi mia moja. Kadi ya maombi K. Ndiyo iliyokuwa, K? K, themanini na tano, nani anayo? Inua mkono wako. Naam, iko mahali fulani? Themanini na tano, njoo papa *hapa*. Themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa, tisini, katika K. Tisini, tisini na tano, mia moja, pangeni mstari hapa chini, huku nikizungumza na wasikilizaji waliosalia, kwa kitambo kidogo.

174 Ni wangapi hapa ambao hawana kadi ya maombi? Nawe ni mwaminifu kweli, na unataka Mungu akusaidie, inueni

mikono yenu. "Si—sina kadi ya maombi, Ndugu Branham." Sasa angalieni. Sasa msisogeesogee. Sh! Hebu wale wanaotoka nje, waje hapa juu, kwa dakika moja tu. Iweni na kicho kwelikweli sasa, dakika chache tu.

175 Wazia, tuko katika Uwepo wa Hakimu wa Mbingu na nchi. Ungekuwa na kicho kiasi gani iwapo ungemwona Yeye akiwa amesimama hapa? Ungekuwa kwenye magoti yako, ukipiga mayowe, kulia, kila kitu. Lakini Yeye yupo hapa. Aliahidi hilo, "Popote watakapokutanika wawili au watatu katika Jina Langu . . . " Hiyo haimaanishi, maana umesema tu, "Hili hapa Jina." Hiyo inamaanisha, " . . . katika Jina Lake, niko miongoni mwao." Angalia.

176 Sasa je! wapo wote, wale nilioita? La. K, themanini na tano, je! hiyo ndiyo niliyoita, ama tisini? [Mtu fulani anasema, "Themanini na tano."—Mh.] Themanini na tano, themanini na tano hadi mia moja, simameni *hapa*. Iwapo huwezi kuja, ninii . . .

177 Yupo mtu kwenye kitanda cha wagonjwa hapa, mtu fulani aiangalie kadi yake. Labda mtu huyo hawezi kutembea. Angalia kama—angalia kama hiyo ni namba yake. Ninaona anayo kadi ya maombi mkononi mwake. Kama ni yeye, mbona, waweza kumwingiza kwenye mstari wa maombi. K, themanini na tano hadi mia moja. Iwapo pana mtu asiyeweza kusimama, labda mtu fulani ni kiziwi; angalieni kote kwenye kadi za mmoja kwa mwenzake. Na wakati mkifanya hivyo, niangalieni huku, nyinyi wengine.

178 Sasa, je! mnaamini kwamba, "Yeye, hapo mwanzo, alikuwa Neno, nalo Neno lilikuwa pamoja na Mungu, nalo Neno lilikuwa Mungu; na Neno likafanyika mwili likakaa katikati yetu"? "Yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaamini hilo? Basi, kile ambacho Neno limefanya daima, liliyatambua mawazo ya moyo. Hiyo ndiyo sababu watu hao walijua kwamba Yesu alikuwa Masihi. Je! hiyo ni kweli? Ni wangapi wanajua hilo?

179 Sasa, kulikuwa na maskini mwanamke, wakati mmoja, ambaye aliamini kwamba kama angeweza kugusa vazi Lake angepona. Je! mnaikumbuka hadithi hiyo? Sasa, kumbukeni, aliamini tu. Yeye alikuwa katika mwili wakati huo.

180 Tena, kumbukeni, Yeye alifanya hivyo mara moja tu. Alimwambia tu huyu mwanamke yale aliyokuwa ametenda; alikuwa na waume wengi kupita kiasi. Nao mji wote wa Sikari ulimwamini Yeye, kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyo, naye akiwa ni kahaba.

181 Na sasa hawataamini kama m—mhudumu mtauwa, aliyeteuliwa na Mungu, pamoja na Injili, anaweza kuwaambia. Wangali hawaamini, hawataamini. Mnaona? Mnaona? Wamepoza kabisa, giza! Kwa kweli, ulimwengu mzima, inaonekana kama una shinikizo juu yake. Ninii tu, sijui jinsi

ya kulieleza, bali liko hapa. Marafiki, amkeni! Wakati umeenda kuliko tunavyodhania.

182 Sasa wewe keti hapo na umtazamie Yeye. Sasa Biblia ilisema, katika Waebrania 4, kwamba, "Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Je! hiyo ni kweli? Sasa ikiwa Yeye ndiye yule Kuhani Mkuu, nawe umemgusa, ungeweza kumgusa kama yule mwanamke alivyogusa. Sasa, Yeye hakuhisi mguso wa kimwili; alisema, "Naona kuwa nimekuwa mnyonge." Nguvu zilimtoka. Sasa kama Yeye angali ni yule Kuhani Mkuu, bado unaweza kuvuta nguvu kutoka Kwake, kwa sababu ni Yeye yule jana, leo, na hata milele.

183 Basi anafanyaje? Kama alivyosema Mungu. Katika siku za Sodoma, ishara ilikuwa ni kitu gani? Mungu, Elohimu, katika mwanadamu, aliyekula, akanywa. Je! mnaelewa hilo? Yesu alikuwa ni Mungu katika mwanadamu. Hiyo ndiyo sababu aliyatambua mawazo yao, Mungu ndani ya mwanadamu! Akalirudia tena, akasema litajirudia tena katika siku za mwisho. "Wakati atakapofunuliwa Yeye, itakuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma." Madazani mara madazani ya Maandiko ambayo yamechunguzwa. Bali haikubidi kuwa na fasiri; Mungu atalifasiri kama ni sahihi. Atathibitisha kwamba ni sahihi. Sasa kuwa na imani na uamini. Neno moja kutoka Kwake lafaa kutosheleza.

184 Sasa, Baba wa Mbinguni, hili ni Neno Lako, kadiri nijuavyo. Sasa yote yako mikononi Mwako, Baba. Ninajikabidhi mwenyewe Kwako, pamoja na wasikilizaji hawa. Jalia iwe usiku wa leo, tukiondoka hapa, jalia tuseme, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, wakati Bwana wetu Yesu, katika umbo la Roho Mtakatifu, alipotunenea tulipokuwa huko?" Tujalie, Baba. Ninaomba katika Jina la Yesu, kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

185 Sasa iweni na imani, aminini. Ninaamini Ndugu Pearry anaenda kuisongeza hii hapa karibu, kwa dakika moja.

186 Na sasa, kumbukeni, watu hawa siwajui. Wao ni . . . Ninawajua hawa wahudumu hapa, ninajua kila mmoja wao, bali sioni yeyote mwingine ninayemjua. Ninajua wapo watu wengine huko nje ambao ningewajua. Kama sijakosea, nafikiri huyu ni Ndugu Pat Tyler anayeketi papa hapa; sina hakika, aliyeketi moja kwa moja . . .

187 Katika mstari wa maombi, kama sininii, unajua sijui chohote kukuhusu, inueni mikono yenu. Ninyi mlio kwenye mstari huu wa maombi hapa, mlio na kadi, ili kuja, inueni mikono yenu. Naam, bwana. Sasa, huko nje, mnajua vivyo hivyo.

188 Sasa huu hapa Ukweli. Kama amefufuka kutoka kwa wafu, basi aliahidi kwamba Mungu angefunuliwa katika mwili wa binadamu. Sasa, haijalishi atanitia upako kiasi gani, hamna budi kutiwa upako na imani kuliamini. Mnaona? Inatuhitaji sote

wawili. Wewe. . . Yule mwanamke aliyegusa vazi lake, ilimbidi kuamini. Angeweza kuendelea tu akipita. Mnaona? Ilimbidi mwanamke huyo kuamini. Mnaona?

189 Ni Mungu! Sasa ikiwa mtu fulani anawazia, "Karama ni kisu ki—kikubwa kirefu. Mungu alikupa karama, unaweza kuichukua na kuikata, na kufanya kile. . . " Unayo mawazo yasiyo kweli juu ya karama. Karama ni kujua jinsi ya kujitoa mwenyewe njiani, na kumwacha Mungu afanye kile anachotaka kufanya. Unaona, ni kujua jinsi ya kujituliza mwenyewe, ili Mungu aweze kukutumia katika njia anayotaka. Jiondoe tu njiani. Unaona?

190 Sasa sijui yeyote wa watu hawa, simjui mtu huyu hapa. Huyu hapa mama amesimama hapa, anaonekana kama wangu wa thamani ambaye ndio kwanza aondoke kwenda Utukufuni, hivi majuzi. Si ningekuwa ni kitu cha kuogofya, kama mama yangu angeweza kuangalia chini kutoka Utukufuni usiku wa leo, awazie kwamba ningekuja hapa kumdanganya maskini mtu kama huyo? Ningekuwa na madhumuni gani? Ningekuwa mwendawazimu. Nipo hapa kujaribu kukusaidia, mama.

191 Na jambo pekee niwezalo kufanya ni kufanya tu lile nililoagizwa kufanya. Siwezi kuwafanya watu kuamini. Siwezi kumfanya yeyote kuamini. Ni kwamba tu, nina . . .

192 Mimi si mwanatheolojia. Mimi hata si. . . mimi si ninii. . . sijiiti mwenyewe mhubiri, mnaona, kwa sababu sina elimu. Mhubiri leo hii ni mtu ambaye ana Digrii yake ya kwanza ya Sanaa na digrii ya Udaktari. Mbona, mimi sijui vitu hivyo ni nini.

193 Mtu fulani aliniuliza hivi majuzi, kasema, "Hutumii nomino zako na viwakilishi nomino ipasavyo."

194 Nikasema, "Sijui ni nini hivyo. Si—sijui." Sikujua nomino ni kitu gani, wala kiwakilishi jina. Nisingeweza kukuambia, kuyaokoa maisha yangu, tofauti kati ya jina na kiwakilishi jina. Siwezi kukuambia.

195 Bali jambo moja ninajua, ninamjua Yeye, Nguvu za kufufuka Kwake. Hayo ndiyo tu ninayojali, mnaona. "Yeye," Ndiye ambaye ninataka kumjua. "Kumjua Yeye, ni Uzima." Na huo ndio ninaotaka, Uzima, kuishi. Huo ndio uliokuleta hapa, Uzima, kuishi.

196 Sasa, mama, kama Bwana Yesu atanifunulia jambo ambalo umefanya, jambo ambalo hukupaswa kufanya, jambo ambalo limekuleta hapa. Kama alivyomfanyia yule mwanamke, akamwambia kilichokuwa ni shida yake; labda niseme shida uliyo nayo, ikiwa kunayo, basi utajua kama ni kweli au si kweli. Utakuwa shahidi wa hilo. Je! hiyo ingekufanya. . . Ungejua kuna Kitu, kitu fulani kilikuwa kimekuja kutoka mahali fulani. Isingeweza kuwa ya kimaumbile. Ingebidi iwe ni ya Kimbinguni. Vema. Je! ingekufanya kuamini kwamba Neno

hili ambalo nimesema, ingekuwa ni Mungu akilifasiri Neno Lake Mwenyewe, basi hiyo ingekuwa ni Mungu akithibitisha?

197 Je! kusanyiko litaamini vile vile? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Iweni na kicho sasa. Sasa kumbukeni, iweni na kicho kabisa.

Mnasema, "Unatapatapa, Ndugu Branham?"

198 Naam, hakika. Simjui mwanamke huyo. Inahitaji iwe ni kitu kingine, Malaika wa Bwana, Roho Mtakatifu Mwenyewe.

199 Ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli kupitia Israeli, Israeli kupitia nyikani. Mnaona, wakati Yeye alipokuwa pale, alikuwa ni Yesu. "Musa alihesabu—alihesabu shutuma la Kristo kuwa ni utajiri mkubwa kuliko ule wa Misri." Aliiacha Misri.

200 Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, alisema, "Naja kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu." Alikufa, akazikwa, akafufuka, akapaa juu.

201 Basi Sauli, njiani akielekea Dameski, aliangushwa chini na Nuru iyo hiyo. Na huyo Myahudi asingeweza kuita nuru fulani isiyojulikana, "Bwana." Naye akasema, "U nani Wewe, Bwana?" Alijua huyo alikuwa ndiye Bwana aliyewaongoza watu wake kupitia nyikani.

202 Akasema, "Mimi ni Yesu." "Yeye yule jana, leo, na hata milele."

203 Sasa ikiwa Nuru iyo hiyo iko miongoni mwetu, mnaona, basi Hiyo inajithibitisha Yenyewe kwa kuzalisha kile ilichofanya kule. Sasa iwapo Yeye atafanya hilo, hilo litatufanya kuamini na kuwa na furaha, sivyo? Naomba alijalie. Wewe ni . . .

204 Ninawatayarisha tu kusema jambo fulani. Mnaona, wakati wewe . . . Wakati unapojiondoa mwenyewe, inakuinua juu; ndipo basi neno lolote usemalo, chochote. Unaona, wewe ni mwanadamu, unayo roho. Na chochote alicho Roho huyo, punde tu anapotia upako, ninaona, ninaweza tu kuona kile kilicho na ni njia gani unaenda kule, kwa ninii . . . Hiyo ni karama ya Mungu. Hivyo ndivyo alivyolifanya, akamwambia yule mwanamke. Jambo lile lile, jambo lile lile hasa.

205 Sasa upo hapa kwa sababu upo kwa niaba ya mtu mwingine. Unataka maombi kwa ajili ya mtu mwingine, naye huyo mtu mwingine yuko hospitalini. Naam. Na ni kifua kikuu. Na huyo ni mume wako. Hiyo ni kweli. Na jambo lingine nililoona, ametiwa uvuli wa mauti. Kuna roho ya giza juu yake, kwa sababu yeye si Mkristo. Hiyo ni kweli. Hiyo si ni kweli? Unaona? Yeye si Mkristo. Ametiwa uvuli wa mauti. Nawe una haja kwamba ampokee Kristo.

206 Pia ninaona umekuwa na tatizo fulani, pia. Ama wanakutarajia kuwa na TB, ama kitu kingine. Jambo ni

hilo, ulifanyiwa eksrei ama kitu kingine. Ndio kwanza wa—wakufanyie eksrei kwa ajili ya TB. Hiyo ni kweli, sivyo?

207 Sasa je! utaenda, kuamini kwa moyo wako wote? Sasa vile tu ulivyoamini, chochote ulichoamini Huyu alikuwa ndiye anayejua hicho sasa, jinsi tu ulivyoamini; mwendee huyo mume, umwambie kilichotukia hapa, na labda roho hiyo ya giza itaondoka; ataokoka, ndipo atainuka na kuja nyumbani. Sasa amini kwa moyo wako wote sasa. Mungu akubariki.

208 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni, unaweza kuihukumu Hiyo vyovyote upendavyo. Ni juu yako sasa.

209 U hali gani, mama? Nadhani hatufahamiani mmoja na mwingine, bali unaamini kwamba Mungu angeweza kunifunulia shida zako? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Basi kama angenifunulia, ingekufanya kuamini kabisa, sivyo? Mwanamume yule alikuja kutoka hapa, ninaona. Uliamini hilo dakika chache zilizopita. La, upo hapa umesimama kwa ajili ya mtu mwingine, pia, huyo ni mume wako. ["Ndiyo, bwana."] Je! unaamini kwamba Bwana Yesu anaweza kunifunulia shida ya mume wako? Je! unaamini? Ana ngiri. Hiyo ni kweli. Na kuna mtoto hapa anayeteseka, unayemwombea, pia. Je! unaamini kwamba hilo litatendeka, pia? Vema. Je! unaamini kwa moyo wako wote sasa? Jinsi tu ulivyoamini, basi na iwe kwa-. . . Unaona, siwezi kuponya. Ninaweza tu kutangaza, unaona, kile nionacho. Nawe amini kwa moyo wako wote, itakuwa kama ulivyoamini. Wewe amini, na Bwana akubariki. Mungu akubariki.

210 Kamwe msitie shaka. Iweni na imani. Wenye kicho kabisa. Sasa kama—kama mkianza . . . Msianze kutembea huku na huku. Mnaona, mmeketi vizuri sana. Kaeni hivyo na msikilize, kwa dakika chache.

211 U hali gani, bwana? Sikujui, hatufahamiani, bali hatuna budi kukutana kwenye Hukumu ya Kristo na kutoa jibu kwa kuonekana kwe—kwetu hapa usiku wa leo. Unaamini hilo, sivyo? Hakika unaamini. Mimi—mimi ninaangalia tu Nuru, bwana, unaona, ni upako, Roho Mtakatifu.

212 Sasa, unasumbuliwa na tumbo lako. Tumbo lako linakutatiza. Hiyo ni kweli. Nawe una jambo unalojaribu kujiondolea, tabia. Na hilo hasa ndilo linalosababisha tumbo lako, itakuwa kansa hivi karibuni sana usipoiacha hiyo, uvutaji sigara. Je! unaamini kwamba Mungu atakuondolea hiyo na kufanya—na kukufanya mzima? Utaamini? Je! unaamini kama nikikuwekea mikono sasa . . . huku hiki Kitu fulani ambacho unajua kinachoonekana cha ajabu kwako? Lakini huo upako wa Kristo, kama nitamwomba Yeye kukuondolea kitu hicho na kukufanya mzima, unaweza kukiweka chini na kuenda zako.

Je! unaamini hilo? [Mtu huyo anasema, "Ninaamini hilo."—Mh.] Njoo hapa. Njoo hapa, bwana.

213 Shetani, juu ya msingi wa imani yetu, Uwepo wa Yesu Kristo Yule aliyekushinda na wote wa jinsi yako, ninamwamuru pepo huyu, anayempeleka mtu huyu kwenye kaburi la mapema, pamoja na hizo sigara, mwondokee, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

214 Nenda sasa na umalizane nayo. Amini, na uishi ikupasavyo.

215 Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Endeleeni tu kuamini.

216 U hali gani? Mama anayeonekana mwema sana, je! unamwamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Sababu ya mimi kusema hayo, wakati Yeye...Je! uliwahi kusoma kitabu changu? Kilisema mle ndani, "Ikiwa unaweza kuwafanya watu wakuamini wewe." Unaona, hilo ndilo jambo kuu, huna budi kuliamini. Wewe umeninii tu...Hakuna njia nyingine ya kumkaribia Mungu ila, kupitia karama, isipokuwa kuiamini.

217 Kama alivyosema Martha, "Na—naamini kwamba Wewe ndiwe Mwana wa Mungu. Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa." Mnaona? Aliiendea vizuri. Wakati, alikuwa na haki kumgombeza kuhusu kukosa kuja, bali yeye hakufanya hivyo. Alikuja kwa kicho, ndipo akapata kile alichoomba.

218 Sasa je! unaamini kwamba—kwamba Mungu yupo na anajua mambo yote? Na unaamini kwamba Yeye anaweza kunifunulia mambo yanayokusumbua? Shida iko kwenye tumbo. Una matatizo, shida nyingi. Pia una matatizo, kivimbe kilichoko tumboni. Hiyo ni kweli kuhusu hicho. Hiyo ni kweli. Vema. Bi Whitley, wewe rudi huko chini, amini kwa moyo wako wote, nawe utapona. Vema. Inashangaza kwamba nilitaja jina lako? Yeye anakujua, pia, unaona.

219 U hali gani? Sasa wewe una tatizo la kike, na hiyo inaonyesha kwamba liko kwenye ovari, na ni uvimbe kwenye ovari. Je! unaamini kwamba Yesu Kristo anaweza kutoa huo uvimbe? Inafaa nikuambie kilichofanyika kwa mke wangu hivi majuzi tu. Unaona, wakati... Ulisikia ushuhuda? Vema, si wako unaweza kuwa kama wake? Vema, utakuwa hivyo ikiwa tu utaamini kwa moyo wako wote.

220 Angalia hapa, msichana. Lako ni tatizo la kike, pia, ugonjwa wa kike. Je! unaamini kwamba Yesu Kristo yupo kukupa afya na kukuponya? Na unaamini basi kwamba yote yatakuwa yamekwisha, na kukuacha kabisa, nawe utakuwa mzima na kuwa...uishi maisha ya kawaida? Vema. Nenda, amini sasa, itakuwa hivyo tu.

221 Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kuponya kisukari, pia, akupe afya? Vema, endelea tu kutembea kupitia jukwaani,

ukisema, “Ninamwamini.” Nacho kitakuacha kama tu ukiamini. Kupewa damu ya Kalvari kutafanya hivyo.

222 Sasa lipo jambo lililotukia kwenye kusanyiko, sikulipata vizuri.

223 Mama anayeketi papa hapa, akiniangalia, anasumbuliwa na tatizo la tumbo. Je! unaamini kwamba Yesu Kristo anakufanya mzima?

224 Moja kwa moja karibu naye yupo mama aliye na tatizo la moyo. Papo hapo nyuma mwenye. . . Moja kwa moja nyuma, amevaa kofia inayoonekana kuwa nyeusi, mwenye ugonjwa wa moyo.

225 Ulikuwa nao, pia. Ulikuwa nao. Unaona, nilisema ulikuwa nao. Nyote wawili mko huru sasa. Yesu Kristo anawapa afya nyote wawili. Vema, ingieni barabarani basi, na Mungu awabariki. Iweni—iweni na imani, aminini kwa moyo wenu wote.

226 Kwenye umri wako, unayo matatizo, mambo mengi yaliyo kasoro. Lakini moja ya mambo makuu unalotaka liombewe, ni moyo wako, pia. Je! unaamini kwamba Yeye atakuponya na ugonjwa huo wa moyo, na kukupa afya? Vema. Nenda, ukiamini hilo, ukisema, “Asante, Bwana,” nawe utapata uponyaji wako.

227 Wasiwasi umemsumbua kwa muda mrefu, ukampa tezi dume, kuamka usiku, bali moja ya mambo makuu uliyo nayo, ni hiki kisukari. Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kukuponya hicho na akupe afya? Endelea tu kusonga, ukisema, “Asante, Bwana Yesu. Ninaamini kwa moyo wangu wote.”

228 Mungu anaweza kuponya aina yoyote ya ugonjwa wa damu, upungufu wa damu, au chochote kingine. Je! unaamini hilo? Vema. Endelea tu, na Mungu atakuponya. Amini.

229 U hali gani? Ninakuona ukijaribu kuinuka kutoka kitandani, pole pole sana, baridi yabisi karibu ikupate. Lakini je! unaamini kwamba atakuacha, usiku wa leo, na sasa unaenda kupona? Endelea tu kutembea kupitia jukwaani, ukisema, “Asante, Bwana Yesu,” na uamini kwa moyo wako wote.

230 Je! unaamini kwa moyo wako wote? Acha aendelee. Aliponywa pale, hata hivyo, kwa hiyo ninii—ninii tu. . . Alishika hiyo, mwenyewe, hata hivyo!

231 Njoo. Je! unaamini kwamba Bwana Yesu anaweza kuponya ugonjwa wa tumbo na kukupa afya, na kukupeleka nyumbani kula? Endelea na uamini hilo, na Yesu Kristo atakuponya.

232 Njoo, mama. Je! unaamini ugonjwa wa mgongo. . .?. . . tatizo, mambo, yatakuacha, unapopitia hili? Endelea kusonga, ukisema, “Ninakushukuru, Bwana Yesu.”

233 Nyinyi nyote mnawazia nini? Je! hili—hili limeyatendea chochote macho yenu, kwa ajili ya siku hii? Je! mnaamini kwa

mioyo yenu yote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu angalia wakienda pale, pamoja na watu!

234 Sasa nyinyi kwenye kusanyiko, aminini, mwone kile Yesu Kristo Mwana wa Mungu, iwapo Yeye angali ni Mwana wa Mungu.

235 Naam, watu hao wanaoenda, wakiketi ndani, wote wana furaha; wakitazamana wao kwa wao, wakishangilia, wakiambiana wao kwa wao kuhusu mambo makuu ambayo Bwana ametenda.

236 Maskini mama aliyeketi hapa, akiugua ugonjwa wa mgongo. Ameketi papa hapa, akiwa na nywele zinazoonekana kuwa na mvi; hapana, huyo mama nyuma yako. Uligusa Kitu fulani, sivyo? Unajua haikuwa ni mimi. Ilikuwa ni Yeye, Kuhani Mkuu. Je! unaamini kwa moyo wako wote, kwamba mgongo wako hautakusumbua tena?

237 Je! ungetaka kuziweka chini hizo sigara, na useme, "Kamwe sitazichukua tena, bwana," mama huyo anayeketi karibu naye? Uliijaribu muda mrefu, bali huwezi kuwa na imani juu yake, kwa njia fulani. Unaamini sasa una imani juu yake? Inua mikono yako ikiwa unasema, "Ninaamini sasa." Vema, usivute sigara tena. Nenda nyumbani ukawe mzima. Fanya ikupasavyo kufanya.

"Ikiwa unaweza kuamini!"

238 Maskini mama anayeketi hapa amevalia koti jekundu, akiniangalia, anayeugua baridi yabisi. Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kukuponya, mama? Unaamini? Vema. Unaweza kupata wako. Vema.

239 Je! hiyo ilikusisimua, dada unayeketi hapo? Mama huyo ana matatizo. Atayakosa. Mungu, nisaidie. Bibi Cox, je! unaamini? Vema. Sikuninii . . . Alidhania angeepuka na hilo, bali hakuepuka. Umeupata, hata hivyo.

Hebu tuseme, "Bwana asifiwe," marafiki. Hivi hamjui . . .

240 Bwana, una kansa, homa ya nyongo ya manjano. Huwezi kuishi, ukilala hapo. Hiyo ni kweli. Sininii, siwezi kukuponya. Bali huwezi kuficha shida yako. Unaona, ipo hapo. Wewe, wewe huwezi kuishi ukiketi hapo, unajua hilo, maana ume—umekwisha. Wanasema iko tumboni mwako, na ndivyo ilivyo. Iko kwenye ini, ambayo inafanya homa ya nyongo manjano kuinuka. Lakini je! unaamini kwa moyo wako wote, na uko tayari sasa, kama wale watu waliokaa kwenye lango kule Samaria, kasema, "Kwa nini tuketi hapa hata tufe?" Utakufa, ukiwa umelala hapo. Unayo fursa moja tu, na hiyo ni kumkubali wakati ukiwa Uweponi Mwake, na uamini kwa moyo wako wote. Je! utafanya hivyo? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, amini kwa moyo wako wote, na usimame, uchukue kitanda chako na uende nyumbani, ukimshukuru na kumsifu Mungu.

241 Je! unaamini hilo? Loo, Mungu atampa nguvu, usifadhaike juu ya hilo. Kama yeye...Huyo hapo, anaenda kuchukua kitanda chake cha wagonjwa, akikunje na kuenda nyumbani.

242 Nyinyi wengine mnaamini? Simameni kwa miguu yenu sasa. Vipi kuhusu nyinyi kusimama? Sijali una shida gani, simama. Inua mikono yako na umpe sifa.

243 Bwana Yesu, wako mikononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo!

*Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua* SWA64-0312
(When Their Eyes Were Opened, They Knew Him)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 12 Machi, 1964, katika Ukumbi wa Munispaa, kule Beaumont, Texas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org